SUPA JACKPOT
TZS. 1,107,465,397
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Dk.** Mwinyi akerwa na upotoshaji nyumba za makazi Kilimani

UKURASA 3




UKURASA 9

Nipashe
MWANGA WA JAMII
Jumapili Aprili 30, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • No. 0581296
www.ippmedia.com
JUMAPILI
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# CAG ashtukia upigaji katika miamala simu

UKURASA 2





Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akimjulia hali Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dk. Festo Dugange, katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Benjamin Mkapa, Dodoma jana, aliyepata ajali ya gari Aprili 26, mwaka huu. **PICHA: TAMISEMI**

UKURASA 3

## Zahanati yafungwa kwa mwaka mmoja madai ya daktari kufariki dunia





## Pinda awageuzia kibao wazazi mmonyoko wa maadili kwa vijana

UK. 2

MICHEZO YANGA YAWAITA WANANCHI UK. 24
MAONI, KATUNI UK.6

# Mtoto afariki kwa Marburg

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema mtoto mwenye umri wa miezi 18 ambaye alikuwa ametengwa na mama yake baada ya kuhisiwa kuwa na ugonjwa wa Marburg, amefariki dunia.

Kifo cha mtoto huyo kimefanya mpaka sasa waliofariki dunia kwa ugonjwa huo tangu kuripotiwa kuwapo nchini kufikia watu sita.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam na waandishi wa habari kuhusu mwenendo wa ugonjwa huo, Waziri Ummy alisema kwa sasa hakuna maambukizi mapya.

Alisema Aprili 4, mwaka huu, alipotoa taarifa ya mwenendo wa ugonjwa huo, walipata ongezeko la mgonjwa mpya mmoja ambaye ni mama wa mtoto wa umri wa miezi 18, aliyekuwa ametengwa na baadae kuthibitika kuwa na maambukizi ya virusi vya Marburg.

"Kwa ujumla, toka tulipotangaza uwapo wa ugonjwa huu mkoani Kagera Machi 14, mwaka huu hadi sasa, jumla ya watu waliopata maambukizi ni tisa.

Waziri Ummy alisema watu 211 kati ya 121 waliokuwa wametangamana na wagonjwa na kuwekwa karantini wameruhusiwa baada ya kumaliza siku 21 za ufuatiliaji bila kuonesha dalili za ugonjwa huo.

"Hii ni ishara kuwa jitihada za pamoja zilizofanyika katika kukabiliana na mlipuko huu zimeleta mafanikio makubwa.

Ninafurahi kuwajulisha kuanzia Aprili 21, mwaka huu, hatuna mgonjwa yeyote mwenye virusi vya ugonjwa huu mkoani Kagera. Wagonjwa wawili waliokuwa wamesalia katika vituo maalum vya matibabu waliruhusiwa kutoka Aprili 20 na 21, baada ya kuthibitika kimaabara kuwa, hawana tena virusi vya Marburg," alisema.

Alisema kwa mujibu wa mwongozo wa Shirika la Afya Duniani (WHO) wa ufuatiliaji wa magonjwa ya mlipuko ukiwamo Marburg, serikali itaendelea kuufuatulia ugonjwa huo.

Ummy alisema endapo hakutatokea mgonjwa mpya mwenye virusi vya Marburg baada ya siku 42 tokea mgonjwa wa mwisho kuthibitika kutokuwa na maambukizi, ifikapo Mei 31, mwaka huu, watatangaza rasmi kumalizika kwa ugonjwa huo.

"Niwaombe wananchi kuendelea kuchukua tahadhari za kinga dhidi ya ugonjwa huu na magonjwa mengine ya kuambukiza, na kuendelea kutoa ushirikiano kwa wataalamu wa afya kadri itakavyokuwa inahitajika,"alisema.

Aidha, Waziri amewataka watoa huduma za afya kuzingatia miongozo ya kuzuia na kudhibiti maambukizi kutoka kwa wagonjwa.

Alisema timu ambayo imewahudumia wagonjwa hao haijapata maambukizi kwa sababu, walichukua tahadhari zote wanazotakiwa kuzifuata.

Katika hatua nyingine, Waziri Ummy akizungumzia kuhusu ugonjwa wa kipindupindu ambao mlipuko wake ulitangazwa mwanzoni mwa wiki hii, alisema hadi sasa hakuna kisa kipya na wagonjwa 13 waliougua wameruhusiwa na wawili wanaendelea na matibabu na hali zao ni nzuri.

Alisema hadi Aprili 28, mwaka huu, jumla ya wagonjwa 15 walitolewa taarifa na wagonjwa 13 walitokea Wilaya ya Ilala na wawili Wilaya ya Kinondoni.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akimpa tuzo maalum Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, wakati wa hafla ya Siku ya Mwanamke wa Bunge, katika viwanja vya Bunge jijini Dodoma, juzi. **PICHA: OWM**.

# CAG ashtukia upigaji miamala ya simu

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini upungufu katika mfumo wa TTMS unaotumiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA) kutekeleza mfumo wa ufuatiliaji wa miamala ya simu za mkononi ili kutoa uhakiki wa mapato.

Katika ripoti yake ya 2021/22 iliyowasilishwa Bungeni hivi karibuni, CAG Charles Kichere, amebaini tofauti kati ya viwango vya malipo vilivyopo kwenye kanuni na viwango vilivyotozwa kutokana na mfumo wa TTMS, kuchukua ada na kodi za miamala ya simu za mkononi kama zinavyotoka kwenye mifumo ya waendeshaji na kutokuwa na udhibiti wa kuthibitisha kuwa mifumo ya waendeshaji inatumia viwango sahihi.

CAG anasema katika Ripoti Kuu ya Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) ya Mwaka 2021/22, upungufu huo unaweza kusababisha malipo ya kodi inayohitajika kuwa ya chini au ya juu.

Aidha, CAG anasema Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania, inahitajika kutekeleza mfumo wa ufuatiliaji wa miamala ya simu za mkononi ili kutoa uhakiki wa mapato kwa kuzingatia Kifungu cha 4 - (2) (i) cha Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Tele-Traffic), 2021.

Kutokana na tofauti katika viwango vya malipo na kodi kwa miamala ya simu za mkononi, CAG anapendekeza TCRA iboreshe mfumo wa TTMS kuweza kukokotoa upya tozo ili kuhakikisha kuwa viwango sahihi vinatumika na kwamba ada na kodi zipo sahihi.

Kuhusu usuluhishi hahifu wa tozo za miamala ya simu za mkononi, CAG anasema ukaguzi ulibaini kuwa na utofauti kati ya kodi zilizoripotiwa katika mfumo wa TTMS wa TCRA na na kodi zilizowasilishwa kwa TRA na waendeshaji.

CAG anasema chanzo cha tofauti hizo kilichangiwa na utaratibu duni wa usuluhishi wa miamala, hivyo usahihi wa kodi za serikali hauwezi kuhakikishwa.

Katika eneo hilo, CAG anapendekeza TCRA iimarishe utaratibu wa usuluhishi kwa kuzingatia taarifa zilizoripotiwa kwa TRA na waendeshaji. Pia itekeleze usuluhishi baina ya mfumo wa TTMS na mfumo wa e-filing wa TRA kwa uthibitisho wenye ufanisi zaidi.

Kuhusu kutokuwepo kwa ufuatiliaji wa miamala ya simu za mkononi isiyofanikiwa. CAG anasema amegundua kuwa ufuatiliaji wa miamala ya simu za mkononi isiyofanikiwa haufanywi katika mfumo wa TTMS.

CAG anasema alielezwa kuwa muundo wa TTMS haukuzingatia miama hiyo, sababu haipaswi kuwa na ada zaidi ya gharama za mtandao zinazohusiana na matumizi ya njia za USSD. CAG anapendekeza TCRA kuimarisha mfumo wa TTMS ili kujumuisha ufuatiliaji miamala isiyofanikiwa yaani Rollback Transactions.

Kadhalika, katika ripoti hiyo ya ukaguzi ya TEHAMA, CAG anasema ukaguzi wa mfumo wa TTMS katika Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano ya Tanzania (TCRA), uligundua tofauti katika viwango vya tozo kwa miamala ya simu, baina ya kiwango kilichotumika na kiwango kilichoanishwa kwenye kanuni, ambapo TTMS inachukua ada na ushuru wa miamala ya simu kutoka kwa mifumo ya waendeshaji bila kuhakiki ikiwa ni sahihi kulingana na kanuni.

Kwa kuongezea, CAG anasema amebaini usuluhishi usiotosheleza kwa ushuru wa miamala ya simu unapelekea kutofautiana kati ya ushuru ulioripotiwa katika TTMS na ushuru uliowasilishwa kwa Mamlaka ya Mapato (TRA) na waendeshaji.

# Pinda awageuzia kibao wazazi mmomonyoko maadili kwa vijana

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda, amesema mambo yanayoendelea hivi sasa kwenye jamii kuhusu mmomonyoko wa maadili kwa vijana wanaopaswa kulaumiwa ni wazazi.

Pia amesema wakati wazazi wakijiuliza nafasi zao za malezi kwa kundi hilo, ndipo waigeukie serikali na kuiuliza nafasi yake katika kuwasaidia vijana.

Pinda ambaye ni Mlezi wa Jumuiya ya Maridhiano na Amani Tanzania, aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa jumuiya hiyo. Alisema yanayoendelea sasa ni mengi na mengine ni ya ovyo ambayo vijana hawapaswi kulaumiwa.

"Lazima tujiulize sisi wazazi, nafasi yetu imekua kubwa kiasi gani katika kuwasaidia hawa vijana halafu turudi tuiangalie serikali na yenyewe tuwaulize, na nyie wakubwa nafasi yenu katika kuwasaidia vijana ipo namna gani? Baada ya hapo tutaona vijana wanabadilika na wanakwenda vizuri,"alisema Pinda.

Alisema wanakoelekea ni muhimu ikaanzishwa idara ya vijana kwa sababu inahitajika na kwamba kijana akielelewa vizuri kwa misingi ya kiimani, atakuwa imara na kwenye jamii atakuwa na amani na utulivu.

"Kama wana maridhiano, tufike mahali siku nyingine tukutane na kuzungumzia mada moja ya malezi ya vijana wetu, maana yanayoendelea sasa unakuta ni mengi na mengine ni ya hovyo na mimi ninasema tusiwalaumu vijana,"alisema.

Kuhusu jumuiya hiyo, Pinda alisema suala la amani, usalama na ulinzi wa taifa ni jukumu la kila Mtanzania.

"Kuwa mzalendo ni kulipenda taifa lako kwa moyo wako na nguvu zako zote, huwezi kukubali mtu kuingilia kati na kuvuruga mweleko. Sisi tupo lakini ni mtu mmoja mmoja, tumeungana na kupata jumuiya ambayo tutakutana na kuambiana ni kwa nini amani tunatakiwa kuilinda kwa nguvu zetu zote," alisema.

Pinda alisema jambo hilo ni kubwa na linahitaji kuhamasisha wananchi ili kutambua umuhimu wa amani na utulivu wa nchi.

"Ukiniuliza nitakuambia tusichezee amani, vurugu zisikie kwa jirani yako huko huko, lakini usiruhusu likaingia nyumbani kwako, ni jambo la hovyo, mnaelewa nchi nyingi zilizoingia katika balaa hili.

"Kurudi katika amani imekuwa ni kazi kubwa na wengine wanahangaika nalo usiku na mchana, sisi Mungu ametubariki tunao viongozi wazuri wanatuongoza vizuri lazima tumshukuru Mungu kwa kuwa na hali hii ya utulivu," alisema.

HABARI KITAIFA

# Zahanati yafungwa kisa daktari kufariki

**Marco Maduhu,** SHINYANGA

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, wamelalamikia kitendo cha Zahanati ya Kijiji cha Bugongwa wilayani hapa kufungwa zaidi ya mwaka mmoja kisa daktari aliyekuwapo kufariki dunia.

Malalamiko hayo yalitolewa juzi kwenye kikao cha Baraza la Madiwani cha Robo Tatu ya Mwaka na kutaka majibu kutoka Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, kuhusu sababu za kufungwa na hatima ya kufunguliwa kwake, ili ianze kutoa huduma za matibabu na kuokoa afya za wananchi.

Diwani wa Viti Maalum, Anna Pius, alisema zahanati hiyo imefungwa mwaka mzima bila kutoa huduma za matibabu kwa wananchi, na kusababisha watu kutembea umbali mrefu kwenda kupata huduma vijiji jirani.

“Wananchi wamekuwa wakifuata huduma za matibabu katika zahanati za vijiji jirani ikiwamo ya Mwamala na Kituo cha Afya cha Samuye,”alisema Pius.

Diwani wa Ilola, Amosi Mshandete, alisema kitendo hicho ni cha aibu na kinamvunja moyo Rais Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa akitafuta fedha kwa ajili ya sekta ya afya ili wananchi wapate matibabu karibu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Nice Munissy, akitoa majibu kuhusu tatizo hilo, alisema hajawahi kupokea taarifa kuhusu kufungwa kwa zahanati hiyo, na kuahidi kulifanyika kazi suala hilo, ili huduma zianze kutolewa.

Baada ya majibu hayo, madiwani walimtaka Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo, Dk. Nuru Yahya, atoe majibu kuhusu kufungwa kwa zahanati hiyo pamoja na, kuliomba radhi baraza kwa nini taarifa hiyo hakuipeleka kwa mkurugenzi.

Dk. Yahya alikiri kufungwa kwa zahanati hiyo huku akisema suala hilo limesababishwa na daktari aliyekuwapo alifariki dunia na kubaki muuguzi peke yake ambaye naye, alipata matatizo ya kifamilia akaondoka, ndipo ilipofungwa.

Alisema hadi kufikia kesho, daktari mwingine atapelekwa ili huduma zianze kutolewa. Dk. Yahya aliwaomba radhi madiwani kuhusu kutofikisha taarifa hiyo kwa Mkurugenzi, akidai alijisahau.



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi, Mohamed Moyo (kushoto), akikagua Kituo cha Afya Namatula juzi, baada ya wananchi kulalamikia uchafu wa mazingira yanayokizunguka kituo hicho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwinyi akerwa upotoshaji nyumba za makazi Kilimani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kuna upotoshaji mkubwa kuhusu nyumba za makazi za Kilimani Mjini Unguja, zilizojengwa zaidi ya miaka 50 iliyopita na Rais wa kwanza, Shekhe Abeid Amani Karume.

Amesema awali alipokea malalamiko kutoka kwa wakazi wa nyumba hizo wakiiomba serikali kusaidia katika ujenzi wa makazi hayo, kutokana na nyumba hizo kuwa chakavu.

Akizungumza jana na waandishi wa habari Ikulu Zanzibar, Dk. Mwinyi alisema wananchi wa eneo hilo walitaka zijengwe mpya kwa kuwa, nyumba hizo ni za zaidi ya miaka 50. Alisema wakisema wazifanyiwe matengenezo gharama ingekuwa kubwa zaidi.

Dk. Mwinyi alisema licha ya eneo hilo la Kilimani kulitumia kwa ujenzi wa nyumba mpya lakini serikali iliamua kujenga kumbi za mikutano ya kimataifa kwa sababu kuna fursa kubwa katika utalii kutokana na ujenzi huo.

Alisema utalii ni roho ya Zanzibar ukihusisha ule wa fukwe na wa mji mkongwe.

“Kuna fursa kubwa ya utalii wa mikutano ambapo duniani utalii huu ni mkubwa, kwa wakati mmoja watu 5,000 huhudhuria na kisha hufanya ziara katika vivutio mbalimbali,” alisema.

Rais Mwinyi alisema wameshafanya mazungumzo na serikali ya Korea ili eneo hilo la Kilimani kujengwe majengo ya mikutano.

“Tukaona hii ni fursa kulitumia eneo la Kilimani kwa maana utalii Zanzibar ni roho ya uchumi wetu, tukiongeza utalii utasaidia maendeleo ya taifa,” alisema.

Rais alifafanua kwamba wananchi wanaoishi kwenye nyumba hizo waliwapa uamuzi wa kuchagua mambo matatu, kuwajengea nyumba mpya zinazofanana na hizo eneo lingine karibu na hapo.

“Chaguo la pili ni kujenga nyumba pembeni ya eneo hilo na kuchangia huduma za pamoja ikiwamo gharama za usafi na utunzaji wa majengo na la tatu, kwa wale ambao hawapo radhi na uamuzi wa serikali, kubaki kuendelea na maisha yao. Lakini kwa bahati mbaya suala hilo likapotoshwa, huu ndo ukweli wa jambo hili, hivyo uamuzi ni wa wakazi waamue wanachotaka,” alibainisha.

Rais Mwinyi alisema kuna watu wanadhani wameipa sekta binafsi kuendesha huduma ikiwamo maabara. “Watu wasipotoshe kuwa kufanya hivyo, wananchi walipie huduma za afya si hivyo, huduma za afya zote zitaendelea kuwa bure,” alisema.

Alisema wanataka kuboresha huduma kupitia sekta binafsi na mlipaji ni serikali.

“Huko kumezagaa maneno ambayo sio ya kweli, na ukweli wenyewe ni huo, shutuma hizo zinatolewa kwa dhamira isio njema,”alisema.

Akizungumza kuhusu fulmonn party ambayo hufanyika ufukweni alisema lazima izingatie mila na desturi na kuhakikisha haibughuzi wingine.

Rais Mwinyi alisema mchakato wa uchunguzi wa watendaji wa serikali waliotajwa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali (CAG), uchunguzi wake ukikamilika watafikishwa mahakamani.

Alisema kuna makatibu wakuu wamesimamishwa kazi kupisha uchunguzi kutokana kutuhumiwa na makosa ya ubadhilifu wa mali za serikali.

Kuhusu uwekezaji katika sekta ya mafuta na gesi, alisema mkakati wa serikali ni kuendelea na utafutaji wa rasilimali hiyo ambapo, kazi hiyo imepewa kampuni ya Rak Gas.

Alisema kampuni hiyo imeshindwa kufanya utafiti ikiwamo uchimbaji wa kisima cha kwanza, kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba wa awali wa utafutaji wa mafuta.

Rais Mwinyi aliitaka kampuni hiyo kutathmini utendaji wake na kumwandikia barua kama wameshindwa kazi hiyo.

## Mbaroni madai kuingiza mbolea bila ya utaratibu

**Na Mary Mosha,** MOSHI

JESHI la Polisi mkoani Kilimanjaro, linawashikilia watu watatu kwa tuhuma za kuingiza mbolea nchini kutoka nchi jirani bila kufuata utaratibu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Simon Maigwa, alisema watu hao walikamatwa Aprili 25, mwaka huu, majira ya 5:00 usiku katika kata ya Rau, Manispaa ya Moshi.

Alisema askari wakiwa kwenye msako, walikamata gari lenye namba za usajili T.390 ACF aina ya Mitsubishi Fuso likiwa limebeba mifuko 141 ya mbolea yenye ujazo wa kilo 50 kila mmoja kutoka nchi jirani pamoja na watuhumiwa watatu.

“Mbolea hiyo iliingizwa nchini na mtu mmoja (jina tunalo) mfanyabiasha, mkazi Moshi na Bomang’ombe wilayani Hai. Upekuzi ulifanyika katika nyumba anayoishi mfanyabiashara huyo pamoja na nyumba ya ndugu yake na kukuta mifuko 36 mingine ya mbolea aina ya Urea Borabora, mifuko 17 ya mbolea aina ya Yara yote ikiwa na ujazo kilo 50 kila mmoja.

“Pia ilikutwa mifuko mitupu 117 ya mbolea aina ya Yara yenye kilo 50, mifuko mitupu 173 ya mbolea aina ya CAN, mifuko mitupu 126 ya mbolea aina ya Borabora, mifuko mitupu 141 ya mbolea DAP, mifuko mitupu yambolea 18 aina ya CAS PLUS, madumu madogo manne, mifuko mitupu 178 ya mbegu za mahindi Hybrid kutoka nchi jirani.


**Summons to appear (O.V, R.20 (1) of (Civil Procedure code)**
**(Substituted service)**
**IN THE COURT OF TANZANIA DAR ES SALAAM**
**(LAND DIVISION)**

**LAND CASE 292 OF 2022**

**KG-INTERTRADE COMPANY (T) LTD..............................................APPLICANTS**

**VERSUS**

**TIB DEVELOPMENT BANK LTD & OTHERS......................................RESPONDENTS**

**TO;**
1. **MELVA INTERNATIONAL LTD**
2. **TRUST COMPANY LTD**

**WHEREAS:** The above named APPLICANT has instituted the **APPLICATION** against you. You are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or authorized Agent on **3RD day MAY, 2023 at 09:00 am Before HON.L.HEMED, JUDGE** to answer the said PLAINT and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your replay.

**TAKE NOTICE** that, in default of your appearance on that day, the said APPEAL will be heard and determined in your absence.

Given under my hand and the seal of this court, this **4th day of APRIL, 2023**

THE HIGH COURT OF TANZANIA LAND DIVISION
DEPUTY REGISTRAR

117404902

# Mahakama yaamuru waliopigwa picha bila ridhaa kulipwa fidia

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam imeamuru Kampuni ya Saruji ya Twiga, kuwalipa wafanyabiashara watano fidia ya Sh. milioni 50 kutokana na kuwapiga picha bila ridhaa yao na kuzitumia katika matangazo ya biashara.

Wafanyabiashara hao ni Christopher Chambo, Eliud Chambo, Fred Roman, Naki Lobora na Yusuf Mgaya. Mahakama hiyo imeamuru kila mmoja alipwe Sh. milioni 10 kama fidia ya kitendo hicho.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Mkuu Evodia Kyaruzi baada ya kujiridhisha kuwa hakuna ubishi kuwa maofisa wa kampuni hiyo, waliwapiga picha wadai hao bila ridhaa yao, na kitendo hicho ni kwamba, kimeingilia utu wa mtu haki yake ya faragha.

"Picha iliyopigwa inaonekana ilikuwa kwa ajili ya kutangaza biashara yao, hivyo kwa kitendo cha kutumia picha bila ridhaa inatakiwa wadaiwa hao walipwe fidia kutokana picha hizo.

"Kitendo cha mtu kutumia picha bila ridhaa ya muhusika mwenyewe inatakiwa alipwe fidia kwa kuwa, bango lililotumika lilikuwa eneo la kiwandani, hivyo mahakama hiyo imezingatia hili," alisema.

Hakimu Kyaruzi alisema kampuni hiyo iliwapiga picha kwa ajili biashara yake na kuonesha huduma zake zilivyo bora, na bango linaonesha kuwa, 'Tunawajali wateja wetu' hiyo ni kuingilia utu wao na haki yao ya faragha, pia haioneshi kama walishirikishwa katika kupigwa picha.

"Wadai hao waliomba kila mmoja alipwe Sh. milioni 500, lakini hawakutoa ufafanuzi kuhusiana na fedha hizo hivyo, mahakama imeamuru kampuni hiyo iwalipe kila mmoja fidia ya Sh. milioni 10 kwa kitendo cha kuwapiga picha bila ya ridhaa na kuzitumia katika matangazo yao ya biashara," alisema.

Mahakama hiyo pia, imeamuru kampuni hiyo kila siku inatakiwa kutoa asilimia saba kama riba ya kimahakama tangu hukumu hiyo ilipotolewa hadi wadai hao watakapolipwa fidia zao.

Awali, Hakimu Kyaruzi alisema wadai hao walikuwa na mashahidi wanne, huku upande wa utetezi waliotoa ushahidi walikuwa watatu katika shauri hilo la madai.

Wadaiwa hao wakiwakilishwa na wakili wao, Richard Kinawali, walifungua shauri hilo la madai namba 141 la mwaka 2020 katika mahakama hiyo wakiomba kampuni hiyo, iwalipe fidia ya Sh. milioni 500 kwa kila mmoja kama madhara ya jumla.

Pia walieleza kuwa, malipo hayo yanayotokana na manufaa yaliyopatikana kutokana na kuchapisha picha zao katika mabango ya matangazo.

Wadai hao ambao ni wakazi wa Dar es Salaam waliomba fidia hiyo kwa madai kuwa, mdaiwa (Twiga Cement) alitumia picha zao bila ridhaa yao na kuzitumia katika matangazo yao ya biashara na vyombo vya habari, ambapo tukio hilo lilitokea 2019.

Katika hati yao ya madai, walieleza kuwa mdaiwa amesajiliwa chini ya kisheria za Tanzania ambapo shughuli zake kubwa ni utengenezaji na uzalishaji wa saruji, ambapo bila ridhaa ya wadai, alitumia picha zao kupanga mikakati ya soko lao, na kujinufaisha kibiashara.

Pia mdaiwa alitumia vyombo vya habari tofauti bila ridhaa ya wadai, kwa kutangaza na kukuza huduma na bidhaa zake kwa kutumia picha zao bila ridhaa yao.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Desderia Haule (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari baada ya mkutano wa mradi wa "Ujana Salama" wa Shirika la Femina Hip, wilayani humo mwishoni mwa wiki. Wengine ni Mwezeshaji Kiongozi wa mradi huo, Stellah Mbuya (fulana ya njano) na Naibu Mkurugenzi wa shirika hilo, Amabilis Batamula (mwenye mkoba mwekundu). Mradi huo, umetoa mafunzo ya kupambana na ukatili wa kijinsia kwa vijana 180 kutoka kata sita za wilaya hiyo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# MOI yatibu maumivu sugu kichwa, mgongo

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa, Upasuaji wa Ubongo na Mishipa ya Fahamu (MOI), kwa kushirikiana na madaktari bingwa kutoka India, kwa mara ya kwanza imetoa huduma ya matibabu ya maumivu sugu ya kichwa na uti wa mgongo.

Kwa siku MOI inapokea wagonjwa 70 wenye tatizo hilo sawa na wagonjwa 1,500 kila mwezi, ambao hupatiwa dawa za kutuliza maumivu lakini sasa watatibiwa tatizo hilo kwa Sh. milioni moja badala ya Sh. milioni 20 iwapo watakwenda nje ya nchi kutibiwa.

Akizungumza na waandishi jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface, alisema huduma hiyo ni ya kwanza kuwapo Tanzania na inatolewa katika maabara ya kisasa ya upasuaji wa ubongo bila kufungua fuvu la kichwa.

Dk. Boniface alisema huduma hiyo ni ya kuwachoma wagonjwa sindano ya kumaliza maumivu katika eneo ambako kuna maumivu sugu na kumaliza tatizo ndani ya saa tatu.

"Huduma hii itasaidia kuepusha upasuaji kwa wagonjwa ambao walikuwa wakitakiwa kufanya hivyo, na huduma hii inatumia saa tatu kwa mgonjwa kufanyiwa na kuruhusiwa," alisema.

Pia alisema huduma hiyo itazisaidia nchi za jirani za Afrika ambako hawana haiko.

Alisema serikali imewekeza mashine za kisasa za kuhakikisha huduma hiyo inatolewa kwa gharama nafuu huku mgonjwa akigharamia dawa na sindano pekee.

Alisema wanashirikiana na wataalam hao wa India ili kujengeana uwezo watalaam wa ndani, kuendesha kambi na kutoa huduma za kimatibabu ya kibingwa nchini.

Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Uti wa Mgongo MOI, Nicephorus Rutabasibwa, alisema huduma hiyo inawahusu wenye maumivu makali kuanzia mishipa ya kichwani hati uti wa mgongo.

Alisema mafunzo waliyopewa yatawasaidia kuendelea kutoa huduma ya matibabu wenyewe hospitalini hapo.

Sababu kubwa ya maumivu sugu, alisema ni uchakavu wa mifupa ya uti wa mgongo na mgonjwa akipatiwa matibabu hayo yanaondoka.

Alisema kambi hiyo ndani ya siku mbili imeweza kuhudumia wagonjwa 18 kati ya 50 ambao walionwa na madaktari.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Tiba ya Utalii, Abdulmalik Mollel, kwa niaba ya mwenyekiti wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Muhimbili, Prof. Mohamed Janabi, alisema huduma hiyo ni moja ya kutekeleza maono ya Rais Samia Suluhu Hassan, ya kuifanya Tanzania kuwa kituo cha utalii tiba za kibingwa katika nchi za Afrika Mashariki.

## Uswisi yaahidi kuvisaidia vyombo vya habari nchini

**Na Halfani Chusi**

UBALOZI wa Uswisi nchini, umesema utaendelea kuvisaidia vyombo vya habari vya Tanzania ili vifikie malengo yake ikiwa ni pamoja kuwawezesha waandishi wa habari kielimu na ufadhili wa kifedha.

Balozi wa Uswis nchini, Didier Chassot, alitoa ahadi hiyo juzi jijini Dar es Salaam, wakati wa mjadala wa pamoja uliowakutanisha waandishi wa habari na wanafunzi wanaosomea taaluma hiyo.

Neema hiyo imetolewa zikiwa zimebaki siku mbili, tasnia hiyo kuadhimisha siku ya uhuru wa vyombo vya habari duniani.

Balozi Chassot alisema waandishi wa habari wanapitia vikwazo vingi ambapo hawana budi kuwaunga mkono kwa kuwapatia elimu na ufadhili wa kifedha ili kufanikisha shughuli zao ikiwamo kufanya habari za uchunguzi.

"Uswisi na Tanzania tuna uhusiano mzuri sana, tumekuwa tukisaidiana kwenye mambo mengi kama ya afya, elimu, usawa wa kijinsia, uendelezwaji wa uchumi na maendeleo ya kisiasa bila kumwacha mtu yoyote nyuma. Lakini pia, kushirikiana kuwalinda na kuwatetea waandishi wa habari Tanzania ambao kwa kiasi kikubwa ndio sauti ya umma kwa miaka mingi.

"Kuwajengea uwezo na mbinu, kuhamasisha usawa wa kijinsia kwenye vyombo vya habari, kupunguzia vikwazo ikiwamo sheria kandamizi, na kuwapa mbinu bunifu zitakazowaingizia kipato kupitia kazi yao,"alisema.

Washiriki wa mjadala huo, walipata fursa ya kuangalia filamu iliyotengenezwa nchini Mexico kwa masaada wa ubalozi huo wa Uswis, yenye kisa cha mwandishi wa habari, Carmen Aristegui, aliyepitia matatizo mengi baada ya kuripoti habari zinazogusa mamlaka ya juu kwenye serikali ya Mexico.

Ilionyesha hali wanayopitia waandishi wa habari kwenye ufanyaji kazi wao, ikiwamo manyanyaso yanayotweza utu wao pamoja na vitisho vyenye ukiukwaji wa haki za binadamu.

Baada ya filamu hiyo balozi huyo alisema, "Wanafunzi mliopo hapa ni matumaini yangu kwamba ujasiri wa Carmen Aristegui, utawatia moyo ili mje kuwa waandishi bora na mahiri kwa nchi yenu.

"Nendeni mkasimamie maslahi ya jamii kupitia vyombo vya habari kama sehemu ya kubadilishana na kujadili hoja mbalimbali na kama chanzo cha habari kwa wote," alisema.

HABARI KITAIFA

# RC aonya wanaotumia wenye ulemavu kuomba

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amewagiza wakuu wa wilaya mkoani hapa, kuwashughulikia wale wote wanaowatumia watu wenye ulemavu kama chanzo cha kujipatia fedha kwa kuwatuma kwenda kuomba fedha mtaani.

Akizungumza jana wakati akizindua Kamati ya Watu Wenye Ulemavu ya Mkoa ambayo imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Na. 9 ya mwaka 2010 ya Watu Wenye Ulemavu, alisema watu hao wanaowatumia walemavu kuomba fedha mitaani zinazopatikana hupelekewa.

"Ninawaagiza wakuu wa wilaya mfanye mchakato wa kuwabaini watu wenye ulemavu wanaojihusisha na kuombaomba, mfanye ufuatiliaji wa kina na kuwachukulia hatua wale wote wanaojihusisha katika kuwatumia watu wenye ulemavu," alisema.

Serukamba alisema kundi hilo linakabiliwa na changamoto mbalimbali katika maisha yao ya kila siku ikiwamo fursa ya elimu, kunyanyapaliwa na jamii, kufichwa na kuonekana ni viumbe duni na kutowashirikisha katika masuala ya kimaendeleo.

Alisema uundwaji wa kamati hiyo ni moja ya mikakati endelevu iliyowekwa na serikali katika kukabiliana na changamoto zinazowakabili na kuongeza uelewa, ufahamu, utambuzi na upatikanaji wa haki kwao.

"Vifungu vya Sheria namba 20 na 22, vinataja Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ndio wasimamizi wakuu wa Sheria namba 9/2010 ya watu wenye ulemavu, hivyo ninatoa agizo kwa wakurugenzi wa halmashauri kupitia viongozi wa vijiji, muweke daftari la orodha ya watu wenye ulemavu ili kuwaibua waliofichwa majumbani," alisema.

Kiongozi huyo alitoa rai kwa viongozi wa serikali na taasisi binafsi, waone umuhimu wa kuwekeza katika kundi hilo kwa kuweka bajeti toshelevu ikiwamo utoaji wa mikopo isiyo na riba na kuwaunganisha katika fursa za kiuchumi na uzalishaji ili wajikwamue kimaisha.

Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, alisema serikali imeunda kamati hizo ili wenye ulemavu wawe na sauti moja katika mambo yanayowahusu na kunufaika na fursa zitolewazo na serikali.

"Viongozi wa serikali kupitia kamati hii tutaweza kupata takwimu za walemavu wote katika mkoa wetu na changamoto zinazowakabili, na hatimaye kushirikiana nao ili waweze kupata fursa kama ilivyo kwa watu wengine," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Watu Wenye Ulemavu Mkoa wa Singida, Sara Nalingigwa, aliishukuru serikali kwa kuendelea kuwajali na kuona umuhimu wa kuundwa kwa kamati hiyo ambayo itakuwa msaada kwao, na kuwaomba wajumbe kumpa ushirikiano ili waweze kufanikisha malengo ya Kamati.



Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu (kushoto), akifungua jiwe la msingi kuzindua mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji, baada ya kujengwa tangi la lita 500000 litakalosaidia wananchi zaidi ya 14000 katika kijiji cha Ubaa, wilayani Rombo, mkoani Kilimanjaro mwishoni mwa wiki. **PICHA: MARY MOSHA**

# Ashauri kuanzishwa sera udhibiti vihatarishi

**Na Restuta James**

SERIKALI imeshauriwa kuwa na sera maalum ya kuangalia vihatarishi kwenye miradi mikubwa ili kudhibiti upotevu wa fedha na kuongezeka kwa gharama za miradi hiyo.

Rai hiyo ilitolewa jana Dar es Salaam na Makamu wa Rais wa Taasisi ya Menejimenti ya Vihatarishi Tanzania (IRMT), Buyamba Buyamba, katika mahafali ya saba.

Alisema iko miongozo ya kuangalia vihatarishi lakini bado wanauhitaji wa sera ili kuzifanya taasisi na menejimenti za serikali na idara zinazohusika na vihatarishi.

Buyamba alisema ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Serikali (CAG), imeonyesha dhahiri kwamba kuna uhitaji wa idara za vihatarishi ambazo zitashughulikia changamoto zinazojitokeza kwenye miradi na kutafuta ufumbuzi kabla ya kutolewa kwa ripoti inayoainisha upotevu wa fedha na hasara ambazo zinapata serikali.

"Serikali kwa sasa inasubiri CAG atoe taarifa baada ya kutokea changamoto,lakini ingekuwa na menejimenti nzuri ya vihatarishi kusingekuwa na ripoti inayoonesha hasara kwa serikali na upotevu wa fedha, tayari wataalam wangekuwa wameshaokoa hasara husika na kwa wakati," alisema.

Alisema miradi mingi inashindwa kufanikiwa kutokana na kutotambua vihatarishi mapema na kuchukua hatua stahiki.

"Sisi tunatoa mafunzo mahususi ya kutambua viashiria maeneo yote hivyo niwaombe Wakurugenzi wa taasisi watenge fedha ili watumishi wao wapate mafunzo madhubuti yatakayowasaidia kupunguza hasara na kuongeza faida kwenye taasisi na kampuni zao," alisisitiza.

Alisema IRMT ipo kwa ajili ya kuisaidia serikali kuhakikisha inatekeleza miradi mikubwa nchini ambayo mara zote inakuwa kwenye hatari ya kupata vihatarishi mbalimbali.

Pia alisema kuwapo kwa taratibu na miongozo itadhibiti viatarishi visiweze kujitokeza na kwamba itabadilisha utamaduni wa kufanya kazi kwa mazoea.

Mtendaji Mkuu wa IRMT, Christopher Njovu, alisema wataalamu wanaozalisha wanalenga kutoa ushauri katika miradi mbalimbali ili kuepuka hasara.

Alisema Tanzania ina zaidi ya wataalamu 500 na ambao wamepata vyeti vya kuwathibitisha ni 126 ambao huweza kusaidia serikali kutopoteza rasilimali zake.

"Ripoti ya CAG imeonesha taifa limepoteza rasilimali hivyo ni fursa kufanya kazi pamoja na taasisi yetu ili kuleta mchango kwa nchi kwani jukumu letu ni kuainisha miradi na tija yake bila upotevu wa rasilimali," alisema Njovu.

Alisema wakiwa kama wataalamu wanaweza kutumiwa kuhakikisha rasilimali za nchi zinakuwa salama na kwa kupitia mpango wa ushirikiano

Njovu alisema hawawezi kutekeleza miradi mikubwa bila kuwa na wataalamu ambao watawasaidia kuleta tija badala ya hasara.

# Jela maisha kwa kusafirisha bangi

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, imemtia hatiani, Ezekiel Kudula, na kumhukumu kifungo cha maisha jela, kwa kusafirisha kilo 198.41 za bangi.

Kudula alitiwa hatiani juzi na Mahakama hiyo, Masijala ya Morogoro, mbele ya Jaji Mustafa Ismail.

Katika hati ya mashtaka, inadaiwa Februari 8, mwaka 2022, Kijiji cha Kitonga wilayani Mvomero, mkoani Morogoro, mshtakiwa alikutwa na gunia (salfet) 10 za majani yanayosadikiwa kuwa dawa za kulevya aina ya bangi, yenye uzito wa kilo 198.41 nyumbani kwake

Wakati akisomewa maelezo ya awali, Machi 21, mwaka huu, mshitakiwa alikana maelezo yote isipokuwa taarifa binafsi ikiwamo jina lake.

Katika shauri hilo, upande wa Jamhuri, uliwakilishwa na Wakili wa Serikali, Messrs Mafuru, huku upande wa utetezi mshtakiwa alitetewa na Wakili Bahati Hacks.

Upande wa mashtaka ulikuwa na mashahidi watano na vielelezo sita.

Miongoni mwa mashahidi hao, Shahidi wa pili, Inspekta Msaidizi wa Polisi Ally Lipinda, alidai akiwa katika ukaguzi usiku, alipokea taarifa kutoka kwa msiri kwamba, bangi inasafirishwa kutoka Kijiji cha Kitonga, wilayani Mvomero.

Askari walifika eneo la tukio, walifanya upekuzi wakiwa na mashahidi na kufanikiwa kukamata gunia 10 za bangi, walimchukua mshtakiwa na kumfikisha Kituo cha Polisi Morogoro.

Mshtakiwa katika utetezi alikana kuhusika na tukio hilo, alidai gunia hizo za bangi zilitoka sehemu nyingine sio nyumbani kwake.

Alidai aliteswa mara baada ya kukamatwa na kwamba, upekuzi nyumbani kwake haukufanyika kwa kufuata utaratibu.

Mahakama baada ya kupitia ushahidi wa pande zote mbili, ilijiridhisha kwamba, dawa hizo zilikutwa nyumbani kwa mshtakiwa.

"Ushahidi wa shahidi wa 2 na 3 hauna shaka kwamba, gunia hizo zilikutwa kwa mshtakiwa, hakuna sababu ya kutokuamini ushahidi wa upande wa mashtaka.

"Ushahidi uliotolewa unanishawishi kuona kwamba, mshtakiwa alitenda kosa analoshtakiwa nalo hivyo Mahakama inamtia hatiani kwa kosa la kusafirisha dawa za kulevya.

"Nimezingatia kumbukumbu za matukio ya nyuma ya mtuhumiwa hazina dosari na umri mkubwa alionao lakini ninapozingatia hayo yote, ninakumbuka uzito wa kosa alilo nalo.

"Kwa kuzingatia athari zake mbaya kwa jamii, nina muhukumu mshtakiwa kifungo cha maisha.

"Adhabu hii itatumika kwa kumkumbusha kuwa uhalifu haulipi, pamoja na adhabu hiyo naamuru kwamba dawa za kulevya, ziharibiwe mara moja,"alisema Jaji Ismail.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe

MWANGA WA JAMII

# Tahadhari ya kipindupindu ichukuliwe umakini mkubwa

**KATIKA** siku kadhaa zilizopita, zilitolewa taarifa kuhusu kuibuka kwa mlipuko wa kipindupindu katika mkoa wa Dar es Salaam huku ikibainishwa kuwa watu 18 walikuwa wamekumbwa na ugonjwa huo.

Pamoja na watu hao kutangazwa kuwa wanaugua ugonjwa huo, ni jambo la faraja kuwapo taarifa kuwa mpaka sasa hakuna kisa kingine kipya na kwamba watu 13 waliokuwa na tatizo hilo wamesharuhusiwa. Habari hizo zilibainishwa jana na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, huku akisema wagonjwa waliobaki ni wawili tu ambao bado wanaendelea na matibabu. Ugonjwa huo uliripotiwa kutokea katika wilaya za Ilala na Kinondoni.

Pamoja na kuwapo kwa habari njema hizo, Waziri aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari za kiafya ikiwamo kuzingatia usafi na kutibu maji kwa kutumia dawa ya Chlorine kwenye vyanzo vyote ili kupata yaliyo salama na kuepuka magonjwa mbalimbali kikiwamo kipindupindu.

Sambamba na hilo, alisema katika mkoa wa Dar es Salaam kuna changamoto ya watu kuwa na visima vifupi ambavyo ni rahisi maji kuwa na kinyesi ambacho ni chanzo kikuu cha watu kuugua kipindupindu. Kutokana na hali hiyo, aliweka bayana kwamba amemwagiza Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, kufukia visima vyote vilivyochimbwa.

Pamoja na hayo, Waziri Ummy alizitaka mamlaka katika mkoa wa Dar es Salaam kuwatoza watu faini kubwa wale ambao wanakiuka maagizo kuhusu kujikinga na ugonjwa huo, ili wanapolipa waone uchungu na hatimaye kutii maagizo kuhusu umuhimu wa afya na hatimaye kujikinga wao na watu wengine. Kuwapo kwa ukiukwaji huo, kumekuwa na hatari katika kipindi cha masika watu kutiririsha maji machafu na hatimaye kuweka mazingira ya kuibuka kwa ugonjwa wa mlipuko, kipindupindu kikiwamo.

Ni dhahiri kwamba katika mkoa wa Dar es Salaam, maeneo mengi ni hatarishi kwa magonjwa ya mlipuko kutokana na watu wengi kujenga makazi bila kufuata sheria za mipango miji. Kutokana na maeneo hayo kuwa katika hali hiyo, kuna hatari kubwa ya kuibuka kwa magonjwa yakiwamo ya mlipuko na yale yanayosababishwa na ukosefu wa hewa ya kutosha kama vile kifua kikuu.

Nyumba hizo ziko katika msongamano mkubwa wa watu, hivyo kuwa katika hatari ya kuibuka kwa majanga mengine yakiwamo ya moto na kusababisha hasara kubwa kutokana na miundombinu mibovu ambayo hairuhusu hata magari ya zimamoto kupita pindi yanapotokea majanga.

Kwa ujumla, Dar es Salaam, kwa muda mrefu, imekuwa 'makao makuu' ya kipindupindu kwa sababu kila inaponyesha mvua maeneo mengi huwa shida kutokana na kuwapo kwa maji machafu huku baadhi ya wakazi wake wakitumia mvua kutiririsha maji machafu kutoka kwenye vyoo vyao. Hatua hiyo huwaweka wakazi wengi hasa kwenye maeneo yasiyopimwa kuwa katika hatari ya kuwapo kwa ugonjwa huo na m engine yanayosababishwa na uchafu.


Ni vyema mamlaka zinazohusika hasa zile za serikali za mitaa, kwa maana ya viongozi wa mitaa, kata, wilaya na mkoa, zikachukua hatua kali dhidi ya wale wote wanaosababisha hatari kuwapo kwa magonjwa ya mlipuko.

Licha ya mamlaka kufanya hivyo, ni vyema pia wananchi wenyewe wakawafichua wale wote ambao wana tabia ya kutiririsha maji nyakati za masika ili wachukuliwe hatua zinazostahili. Ni imani kwamba kama kila mtu atawajibika ipasavyo, Dar es Salaam bila kipindupindu inawezekana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kipindupindu sasa kimebisha hodi, tukuchukue tahadhari

Na Sabato Kasika

**UGONJWA** wa kipindupindu umebisha hodi wilayani Ilala jijini Dar es Salaam, huku Wizara ya Afya ikisema kuwa tayari watu 10 wamethibitika kuugua tangu uliporipotiwa Aprili 20, mwaka huu.

Maeneo yanayotajwa kukumbwa na ugonjwa huo ni Kivule ambapo watoto wawili wa familia moja walithibitika kuwa na dalili za ugonjwa huo, watu wanne wa familia moja pia wamethibitika kuwa na dalili.

Kwa taarifa hiyo, ni vyema kila mmoja wetu kuchukua tahadhari ili kuwa salama dhidi ya ugonjwa huo, ambao unatajwa na wataalam wa afya kuwa unaua kirahisi, lakini pia ni rahisi kuuepuka.

Kutokana hilo, ni wazi kila mmoja wetu akichukua tafadhari kwa kufuata maelekezo ya wataalam wa afya, anaweza kuwa salama kwa kuepuka ugonjwa huo wa mlipuko.

Inaelezwa kuwa rafiki wa kipindupindu ni uchafu, na kwamba mtu akizingatia usafi, hasa katika kuandaa vyakula, kuchemsha maji ya kunywa, kunawa maji kwa kutumia sabuni baada ya kumaliza huduma ya maliwato na kutokula vyakula vya baridi, anakuwa salama.

Ni vyema kuzingatia usafi iwe nyumbani na kwingineko, kwani inaelezwa kuwa kuna athari kubwa ambazo zinaweza kusababishwa na ugonjwa huo, hivyo ni muhimu kuchukua tahadhari.

Dar es Salaam ni miongoni mwa mikoa ambayo kipindupindu kimekuwa kikipotea na kurudi, ninadhani hii inaonyesha baadhi ya watu hawajazingatia umuhimu wa kulinda afya zao.

Kwa kuwa tayari tumetangaziwa kuwapo kwa ugonjwa huo jijini Dar es Salaam, jambo la msingi ni kuchukua hatua za kutuweka salama Ili tusiwe marafiki wa kipindupindu.

**Wataalam wa afya kuwa wanasema ugonjwa huo husababishwa na bakteria aina ya vibrio cholera kwenye utumbo mwembamba, ambaye hutoa sumu na kuchangia kutolewa kwa maji mengi ndani ya utumbo, kwa njia ya kuhara, wakati mwingine kutapika na homa kali.**

Wataalam wa afya kuwa wanasema ugonjwa huo husababishwa na bakteria aina ya vibrio cholera kwenye utumbo mwembamba, ambaye hutoa sumu na kuchangia kutolewa kwa maji mengi ndani ya utumbo, kwa njia ya kuhara, wakati mwingine kutapika na homa kali.

Katika ufafanuzi wao ni kwamba, bakteria huyo anapatikana katika chakula au maji machafu na kinyesi kutoka mtu aliye na maambukizi, na pia mtu anaweza kuambukizwa kupitia maji machafu, mboga zilizopandwa kwenye majitaka, samaki waliovuliwa katika machafu, vyakula na vinywaji vilivyo na bakteria huyo kutokana na uchafu.

Hivyo, kwa usalama wetu, ni vyema kujitafakari na kisha kuchukua hatua sahihi za kutuwezesha kujilinda dhidi ya ugonjwa huo, kwani inawezekana kuwa salama kwa kuzingatia usafi.

Mama lishe na baba lishe nao hawana budi kuzingatia usafi katikati maeneo yao ya biashara, kutokana na ukweli kwamba baadhi yao huwa hawazingatii usafi katika maandalizi na upikaji wa vyakula.

Wakizingati usafi watakuwa wamelinda afya zao na za wateja wao pia dhidi ya ugonjwa huo ambao umekuwa na kawaida ya kuondoka na kisha kurudi tena jijini Dar es Salaam.

Kwa kuwa rafiki wa kipindupindu ni uchafu, basi ni vyema tusikubali kukaribisha uchafu, kwani ugo njwa huo unaweza kuendelea kuwa tatizo katika jamii tusipochukua tahadhari zote zinazotakiwa.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Pongezi VETA kwa kubuni VETA Day



Pascal Mayalla

MAMLAKA ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Tanzania (VETA) licha ya kuwapatia Watanzania elimu ya ujuzi kama nia na dhamira ya serikali kuwezesha wananchi, hasa vijana kuajirika kwa urahisi, kuongeza tija ya uzalishaji viwandani na kuchangia vyema katika maendeleo ya uchumi imeibua jambo kubwa kuliko la kushindanisha wahitimu wake katika mashindano ya umahiri kupitia siku inayoitwa VETA Day, ambayo imeyang'arisha Maonyesho ya Ubunifu Kitaifa yaliyofanyika Dodoma.

Oktoba, 2022 wakati akizindua Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Kagera, Rais Samia alisema: "Tunazungumzia tatizo la kutokuwa na ajira, tunasomesha watoto lakini hawana ajira. Kazi yetu ni kuhakikisha tunawajengea uwezo vijana kwa kuwapatia ujuzi ili waweze kujiajiri na kuajiriwa,"

Na baada tu ya kauli hiyo ya Rais, VETA ikaamua hakuna kulala. Kwanza ikakamilisha kujenga kwa kasi ya umeme, vile vyuo vilivyokuwa kwenye ujenzi na sasa VETA ina vyuo 50 vilivyokamilika, vinavyotoa mafunzo ya ufundi stadi Tanzania. Kisha ikaanza ujenzi wa vyuo vipya 33. Vyuo 29 ni vya ngazi ya wilaya na vyuo vinne vya ngazi ya mkoa kuanzia Samia alipoingia madarakani mwaka 2022 hadi sasa kazi inaendelea.

Kazi hiyo, kubwa na nzuri, serikali imetumia Sh. bilioni 94.5 katika kuwezesha ukamilishaji wa ujenzi wa vyuo hivyo. Sasa vyuo hivyo vinatarajiwa kuleta ongezeko la Zaidi ya wanafunzi 40,000 katika udahili kwenye vyuo vya VETA.

Moja ya sifa kubwa za VETA, si tu kutoa mafunzo mbalimbali ya ufundi stadi, bali pia ujenzi wa vifaa mbalimbali kwa matumizi. Mfano kwenye vyuo vipya vyote, VETA imetumia samani mbalimbali 30,750 zilitengenezwa na VETA kwa ajili ya vyuo hivyo.

Utekelezaji wa mradi huo wa uzalishaji samani za vyuo, umetoa zaidi ya ajira 15,000 kwa wananchi Watanzania na vyuo hivyo vitakapoanza kutoa mafunzo, inatarajiwa kutoa zaidi ya ajiora 1,000 za moja kwa moja.

Vijana wa Kitanzania wanaojiunga na mafunzo kwenye vyuo vya VETA wanalipa ada ya Sh. 120,000 tu kwa mwaka kwa wale wanaokaa bweni na Sh. 60,000 kwa mwaka kwa wale wanaohudhuria mafunzo kwa kutwa kwa mwaka. Gharama zingine za mafunzo hulipwa kwa ruzuku ya serikali.

Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imeendelea kutekeleza programu mbalimbali za kuwawezesha wananchi wa makundi mbalimbali kujipatia ujuzi. Mfano, kupitia Mpango wa Uanagenzi ulioratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) zaidi ya vijana 10,000 walimefadhiliwa kupata mafunzo katika vyuo vya VETA.

Takwimu za hivi karibuni zinaonyesha asilimia 75 ya wahitimu wa ufundi stadi wanaajirika. Mfano asilimia 32 ya wahitimu wa VETA, wameajiriwa kwa ajira rasmi, huku asilimia 38 wakijiajiri.

Wahitimu wa VETA waliobaki ni ama wanajitolea, wanaendelea na masomo au wanafanya kazi kwenye karakana za familia.

Ufundishaji na ujifunzaji wa ufundi stadi mara nyingi huchochea ubunifu. Mafunzo ya ufundi stadi yanayotolewa na VETA, yanawajengea walimu na wanafunzi utamaduni na ari ya kubuni teknolojia mbalimbali kwa ajili ya kutatua changamoto mbalimbali katika jamii na kurahisisha shughuli za kiuchumi.

Kwa hiyo VETA iliamua kubuni mbinu ya kukuza ubunifu kupitia Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU). Toka mwaka 2019 hadi mwaka jana, wabunifu 82 kutoka vyuo vya ufundi stadi na wabunifu 573 kutoka mfumo usio rasmi walitambuliwa. Shindano la Ubunifu la VETA Day, limeyashamirisha sana Maonyesho ya mwaka huu ya Ubunifu Kitaifa katika uwanja wa Jamhuri, Dodoma.

Kwa mantiki hiyo, VETA imekuwa ikisaidia uendelezaji wa ubunifu wa walimu na wanafunzi wa ufundi stadi, pamoja na wale walio katika mfumo usio rasmi kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na, kwanza ni kwa kuwaunganisha na kuwadhamini kupata ufadhili wa Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH) na pili, kuwawezesha kifedha kwa vyanzo vyake vya ndani, pamoja na kuwapatia nyenzo na vifaa kwa ajili ya kuendeleza ubunifu wao.

Tatu, VETA kwa kuzitangaza rasmi ubunifu kuwatangaza na kuwaunganisha na taasisi na mashirika mengine yanayosaidia uendelezaji ubunifu. Pia VETA kwa kushirikiana na wadau, imekuwa ikitenga fedha na kuratibu uendelezaji wa wabunifu wa ufundi stadi.

Kupitia MAKISATU wabunifu 10 Bora wamekuwa wakiwekewa utaratibu wa kuendelezwa na Serikali kupitia COSTECH. Hakuna nchi inayoweza kupata maendeleo bila ubunifu wa kubuni bidhaa zake na kuzitumia kujiletea maendeleo ya kweli ambayo ni maendeleo endelevu.

Hivyo ndivyo wenzetu wa ulaya ndio walioanza Mapinduzi ya Viwanda (Industrial Revolution), Marekani ikaja kuwapiku kwa teknolojia, China ikaja kufunga kazi kwa kutengeneza kila kitu.

Hivyo Tanzania tukiamua kwa dhati kukuza ubunifu, iko siku tutatoka.

Mungu ibariki Tanzania.

**Paskali**
**+255 754 270403**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Alichokifanya Samia kwa Hamimu kitalipwa peponi



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

**Hamimu ni kijana mdogo wa miaka 15 tu, aliyepitia kipindi kigumu sana cha ugonjwa wa ngozi na kama si Rais Samia kumwona kijijini kwao Nyakanazi, Biharamulo mkoani Kagera Oktoba 16 mwaka jana, asingekuwa kama alivyo leo.**

WAKATI naanza kujitambua miaka hiyo, nikihudhuria mikutano baadhi ya hadhara, wahudhuriaji tulikuwa tukisikiliza hotuba au burudani na kujikuta tunashangilia bila kuambiwa wala kuhamasishwa.

Hiyo ilitokana na hisia zilizotugusa ama kwa kuvutiwa na maneno ya kwenye hotuba, au maudhui na mirindimo ya burudani zitolewazo na mtu au kikundi cha watu katika matukio husika.

Lakini siku hizi kushangilia kama huko kumekuwa nadra sana, kwani leo watu wanahimizwa kushangilia. "Haya jamani shangilieni, mpigieni makofi au jamani nipigieni makofi!"

Hiyo inakuja hata kama lililozungumzwa haligusi hisia za hadhira au hata kama maudhui na mirindimo ya burudani itolewayo havigusi nyoyo za waliopo, ili mradi mtu anataka kuonesha kuwa kilichosemwa au kuimbwa ndicho.

Furaha au kuridhika ni hisia mwilini mwa mtu, kwamba mtu atafanya jambo la furaha kutokana na kuguswa, halikadhalika atachukia kutokana na hisia za chuki dhidi ya matakwa yake.

Mimi kwa kweli hivi karibuni nilipatwa na hisia ya kufurahia jambo na nikashangilia kwa kupiga makofi, baada ya kusoma na kuona, kwamba Rais Samia Suluhu Hassan amekutana na kijana Hamimu Baranyikwa.

Hamimu ni kijana mdogo wa miaka 15 tu, aliyepitia kipindi kigumu sana cha ugonjwa wa ngozi na kama si Rais Samia kumwona kijijini kwao Nyakanazi, Biharamulo mkoani Kagera Oktoba 16 mwaka jana, asingekuwa kama alivyo leo.

Kwa mujibu wa simulizi ya kijana huyo, alipatwa na matatizo hayo muda mrefu uliopita, akahangaika sana kupata matibabu, ikiwa ni pamoja na wazazi kuuza mali ili kumgharimia, lakini ilishindikana.

Anasema hatua hiyo iliwakatisha tamaa wazazi wake na kusema wameishia hapo na kumwachia Mungu, huku Hamimu akisema basi liwalo na liwe na wamwache tu aumalize mwendo, kwani kwa umasikini wao asingefanya lolote.

Hata hivyo, Mungu wake akasema si muda mwafaka kumchukua kijana mdogo kama huyo, huku kukiwa na fursa ya kutokea mtu kuokoa maisha yake. Siku ya ziara ya Rais Samia, Mungu akamwamsha Hamimu alfajiri akampeleka barabarani.

Kwa mwongozo wa Mungu wa Rais Samia ambaye bila shaka ndiye pia wa Hamimu, akajikuta machoni mwa Rais ambaye bila kusita, hisia zikamfika na kuagiza akatibiwe kwa gharama zake (Rais).

Maagizo ya Rais yakamfikisha Hamimu katika hospitali ya Taifa Muhimbili, Dar es Salaam, ambako juhudi za madaktari na wauguzi zilifanikiwa kumvua koti la umauti alilokwishalitamani.

Na aliporuhusiwa baada ya kuonesha maendeleo mazuri kiafya, Hamimu akaomba amwone mwokozi wake angalau alivyo, ili apate kumshukuru kwa hilo kubwa alilomfanyia katika historia ya maisha yake.

Kwa urahim wa Rais Samia, akalisikia ombi hilo na kuruhusu Hamimu afike Ikulu, Dar es Salaam na akafanikiwa kumwona kwa mara ya kwanza Rais wake aliyemkomboa. Hakuamini macho yake.

Bila shaka Hamimu alijiuliza yeye ni nani mpaka apewe heshima ya kuingia Ikulu na kuonana na Mkuu wa Nchi, fursa ambayo si rahisi kupatikana kwa mtu wa kawaida na fukara kama Hamimu.

Tukio hili la Hamimu na Rais Samia, linatufunza mengi kwamba madaraka si kibali cha kudharau masikini, utajiri si njia ya kudhihaki asiye nacho na kupuuza kilio chake ilhali una uwezo wa kumsaidia.

Hamimu alisema kijijini kwao, kuna watu wenye uwezo mkubwa na ukwasi uliopindukia, lakini hawakufumbua macho kumwona wala kuzibua masikio kumsikia Hamimu na kumsaidia. Ila Rais Samia aliweza. Marais wangapi wamefanya au hufanya hivi?

Si mara ya kwanza Rais Samia anafanya hivi, ikumbukwe alimgharimia msanii na Mbunge wa zamani Joseph Haule, 'Profesa Jay' aliyelezwa Muhimbili mpaka akatoka akiwa timamu licha ya kwamba ni mpinzani kisiasa.

Hatua hii ya Rais inazidi kudhihirisha moyo alionao Rais Samia, moyo wa kuhurumia na kujali maisha ya wengine bila ubaguzi wa dini, kabila wala itikadi, akiamini kuwa wote ni Watanzania. Mungu atamlipa, Ishallah!

Wenye uwezo wa kusaidia, wasaidie wasio na uwezo bila kusubiri kutangazwa kwa ajili ya kiki, bali waelwe kufanya hivyo ni sawa na kumsaidia Mungu kulea viumbe wake na hakika mwisho wa maisha, watashukuriwa hata mbinguni.

**Alamsiki!**

# Watakiwa kusimamia wataalamu utekelezaji miradi ya kimkakati

Na James Mwanamyoto

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, amewataka wakurugenzi, wakuu wa idara, mameneja na maofisa wanaosimamia utawala na rasilimali watu katika taasisi za umma kuwasimamia vyema wataalam na watumishi wa umma waliopewa dhamana ya kutekeleza miradi ya kimkakati ya serilikali.

Amesema hatua hiyo itawawezesha wananchi kunufaika na miradi kama ilivyokusudiwa na Rais Samia Suluhu Hassan ambaye anaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali.

Kairuki alitoa wito huo jana kwa wasimamizi wa utawala na rasilimaliwatu Dar es Salaam wakati wa kufunga Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Jumuia ya Wataalam wa Utawala na Rasilimaliwatu Afrika (AAPAM) Tawi la Tanzania kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene.

Alisema wataalamu hao ndio wenye jukumu la kuhakikisha waliopewa dhamana ya kusimamia miradi ya kimkakati, wanatekeleza kwa wakati, uadilifu na kwa kuzingatia ubora ili iwe na manufaa kwa wananchi na taifa kwa ujumla.

"Mtakubaliana nami kwamba mnalo jukumu kubwa la kuhakikisha wataalam wetu na watumishi wanaofanya kazi ya kutekeleza miradi mbalimbali wanaisimamia kwa uadilifu, ufanisi na weledi ili wananchi wanufaike na uwekezaji unaofanywa na serikali katika miradi ya kimkakati na maendeleo," alisema.

Kairuki amesema ofisi yake itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais-UTUMISHI katika kuishauri serikali kuhusiana na masuala ya usimamizi wa rasilimaliwatu ili kuwa na rasilimali watu itakayotoa mchango katika utoaji wa huduma bora kwa wananchi na maendeleo ya taifa.

Pia aliwataka wataalam hao wa utawala na usimamizi wa rasilimaliwatu kutoka katika taasisi za umma nchini kutumia ujuzi na weledi wao kuishauri Serikali namna bora ya usimamizi wa rasilimaliwatu.

Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Juma Mkomi, alisema ofisi yake inatarajia mkutano huo wa AAPAM utaongeza ufanisi wa utendaji kazi kwa wasimamizi hao wa masuala ya utawala na rasilimaliwatu nchini. "Mkutano huu utakuwa na msaada mkubwa kwa Ofisi ya Rais- UTUMISHI katika kuyatafutia ufumbuzi masuala mbalimbali ya kiutumishi ambayo yamekuwa yakilalamikiwa na wananchi na wadau wa taasisi zetu za umma," Bw. Mkomi amefafanua.

Mkomi aliwataka wakurugenzi, wakuu wa idara, mameneja na maofisa wanaosimamia utawala na rasilimaliwatu katika taasisi za umma kuhakikisha makatibu muhtasi hawajikwezi na kuwa kikwazo kwa wananchi na wadau wanaofuata huduma katika ofisi zao.

Mwenyekiti wa AAPAM Tawi la Tanzania, Leila Mavika alisema uongozi wake uliona ni vyema kufanya mkutano mkuu wa mwaka ambao ulikuwa haujafanyika kwa muda mrefu, lengo likiwa ni kubadilishana uzoefu katika usimamizi wa masuala ya utawala na rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma.

Mavika alisema mkutano huo umewashirikisha wajumbe 281 kutoka katika wizara, mamlaka za serikali za mitaa, idara zinazojitegemea, wakala za serikali na taasisi za umma.

## Uchenjuaji madini vyanzo vya maji wapigwa marufuku

Na Ambrose Wantaigwa, TARIME

MKUU wa Wilaya ya Tarime, Michael Mntenjele, amepiga marufuku shughuli zote za uchenjuaji wa madini ndani ya vyanzo vya maji, na kuwataka wananchi wote kuondoka mara moja.

Pia ameagiza idara ya mazingira wilayani hapa, kusimamia uchimbaji wa Mialo nje ya vyanzo vya maji, kwa ajili ya wakazi na wachimbaji wadogo ili kufanya uchenjuaji salama.

Agizo hilo alilitoa katika kikao cha wadau wa maji wilayani hapa kilicholenga kujadili utekelezaji wa miradi ya maji na kuwakutanisha viongozi wa vijiji na wasimamizi wa jumuiya za maji kutoka kata.

Alisema katika kutekeleza miradi ya maji serikali imetoa Sh. bilioni 4.5 kwa ajili ya kutatua kero ya wananchi hasa wanawake ambao hutembea umbali mrefu kutafuta huduma ya maji safi na salama.

"Ni marufuku wananchi kufanya shughuli za kuchenjua madini ndani ya vyanzo vya maji kwa sababu hatua hiyo, inasababisha uharibifu wa mazingira na pia, huathiri afya za watumiaji katika maeneo hayo," alisema.

Katika hatua nyingine, amewataka viongozi wa kata na vijiji kusimamia ulinzi wa vyanzo vya maji na kuwachukulia hatua za kisheria wananchi wanaoharibu

Kiongozi huyo amewaagiza wasimamizi wa mazingira kuhamasisha taasisi za serikali, shule na mashirika yasiyo ya kiserikali kupanda miti kwa wingi maeneo yao ili kulinda mazingira.



Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Halima Dendego (wa pili kulia), akitazama wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mtwivila wakitumia mojawapo ya kompyuta walizopewa msaada na Taasisi ya Vodacom Tanzania Foundation ikiwa ni sehemu ya mradi wa uunganishwaji wa shule za sekondari unaolenga kuziunganisha shule 300 nchini kwa kushirikiana na African Child Projects na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF). Taasisi hiyo, ilikabidhi kompyuta 31 na vifaa vingine vya TEHAMA vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 89 kwa shule 14 za sekondari mkoa huo, mwishoni mwa wiki. Wengine ni Mkuu wa Vodacom Nyanda za Juu Kusini, Happiness Shuma (kulia), Meneja wa Maduka, Dorice Wambagi (kushoto) na Msimamizi wa Ripoti, Pendo Mongi. PICHA: MPIGAPICHA WETU

# Kamishna asisitiza uhusiano mwema huleta tija na ufanisi mahali pa kazi

Na Christina Haule, MOROGORO

KAMISHNA wa Kazi, Susan Mkangwa, amesema uhusiano mwema kazini ni chachu katika kuleta mshikamano na ushirikiano katika kuzuia migogoro ya lazima na isiyo ya lazima, hivyo kusababisha tija na ufanisi katika taasisi.

Mkangwa alisema hayo juzi alipokuwa akizindua warsha ya maofisa rasilimali watu iliyoandaliwa na Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO).

Warsha hiyo ilikuwa na kaulimbiu 'Tija na Ufanisi ni Matokeo ya Uhusiano Bora Kazini. Pamoja Tujenge na Kimarisha Taasisi Zetu.' Awarsha hiyo ilikuwa sehemu ya kuelekea sherehe za Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) itakayofanyika kitaifa kesho mkoani hapa.

Alisema TUICO ina nafasi ya kupongezwa kwa ubunifu wa kufanya warsha za namna hiyo mara kwa mara huku akivitaka vyama vingine vya wafanyakazi kuiga mfano huo ili kuleta uhusiano mzuri kwa mustakabali wa maendeleo ya taasisi ili kuongeza ufanisi katika maeneo ya kazi.

"Kitendo cha kuwakusanya maofisa rasiliamo watu na waajiri na kuwapa mafunzo ya kuimarisha uhusiano sehemu ya kazi kwa kweli hata sisi watendaji wa serikali tunaosimamia sheria za kazi kimetupa moyo na tumejiskia vizuri.

Tunaimani kwamba watu hawa waliokusanyika hapa ndio muunganiko mkubwa kati ya mwajiri na mfanyakazi. Kwa hiyo hata sisi wanatusaidia katika majukumu yetu ya kila siku ya kusimamia utekelezaji wa sheria za kazi katika maeneo yao ya kazi," alisema.

Pia aliwataka kushiriki kikamilifu na kuwa na uhusiano mwema ili kuleta tija na ufanisi katika maeneo ya kazi kwa kuzingatia mada mbalimbali zitakazotolewa zinazolenga kukuza uelewa wa washiriki kuhusu uhusiano mwma, ufungaji wa mikataba ya hali bora na utatuzi wa migogoro ya kikazi.

Mkangwa pia alisema dhana ya uhusano mwema inajumuisha pande mbili au tatu katika ajira na kwamba ni lazima kuwe na mnyororo kati ya mwajiri, mwajiriwa, vyama vya wafanyakazi pamoja na waajiri.

Aliwataka maofisa rasilimali watu kuwajibika katika kuleta uhusiano mwema kwa sababu wakati mwingine wamekuwa wachochezi wa migogoro kuliko hata waajiri.

Pia alisema kuwezesha ufungaji wa mikataba bora, utekelezaji wa mikataba ya Shirika la Kazi Duniani (ILO) na sheria za kazi zilizopo nchini, husababisha kushughulikia malalamiko na migogoro kwa urahisi na kuweka majukumu ya majadiliano ya utatu.

Alisema migogoro iliyoripotiwa Julai 2022 hadi Aprili, mwaka huu, mingi inaongozwa na sekta za ujenzi, ulinzi binafsi, vyakula vinywaji na hoteli, biashara na usafirishaji.

Mkangwa alisema kubainika kwa vyanzo vinavyoongoza katika migogoro ya kikazi, kutasaidia kujiimarisha katika kupata mbinu bora na kutekeleza au kuzuia migogoro katika maeneo hayo.

Naye Katibu Mkuu wa TUICO, Boniface Nkakatisi, alisema malengo ya warsha hiyo ni kuweka ukaribu na kufanya majadiliano badala ya kurumbana na kupelekana mahakamani sababu katika kukaa na kuzungumza hakuna kitu kisichowezekana.

"Ni muhimu vyama vyote vikapenda kuwa na majadiliano na sio matumbano ya kupelekana mahakamani, sababu tunafanya vitu kwa manufaa yetu na nchi yetu" alisema Nkakatisi.

Naye Afisa Mtendaji Mkuu wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Susan Ndomba, aliwataka maofisa uhusiano kujenga tabia ya kuimarisha uhusiano baina yao na waajiri ili kuleta utulivu utakaoleta ufanisi na tija sehemu za kazi.

Alisema ili wafanyakazi wafanye kazi wakiwa vichwa vyao vimetulia wanahitaji uhusiano uwe mazuri, ofisa rasilimali watu anapaswa kuwa makini kuangalia taarifa zipi anapeleka kwa wafanyakazi na zipi anapeleka kwa uongozi.

# MAISHA

APRILI 30, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 14


## JUISI YA UKWAJU

## MAISHA NI NYUMBA




Ukurasa 15

Epuka nyumba yako kutitia baada ya muda mfupi kwa kufanya haya




## KATUNIKA

Ukurasa 16




# RUDISHA UREMBO

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| T | | S | H | A | K | A |
| H | | | | K | | S |
| A | | N | Z | I | | H |
| W | A | O | | L | A | O |
| A | | N | O | A | | N |
| B | | D | | | | W |
| U | B | O | S | I | | E |

## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


KAA, MBA, BUU, MTI, AWEKE, CHOTA, OBAMA, KUMBE, ASHINDE, PAMBANA

## AMSHA AKILI

TAFUTA NJIA KUTOKA A KWENDA B




## TOA TOFAUTI 5



## WATOTO

# PAKA RANGI







KICHEKESHO

HAKUNA watu wenye ndugu wengi kama makonda wa daladala. Ebu msikie konda huyo wa Posta kwenda Makumbusho.

"Haya dada hapo mbele, mjomba kule mwisho kaa vizuri...oyaa mamdogo unaenda? Bibi shuka taratibu, shemeji umeikuta haya panda. Babu njoo ukae!

Baba angu hapo tusogee kidogo,"

"Shangazi maliza ngazi,Swaiba geukia mbele,

Kaka hapo shika upande wa pili,mdogo wangu mpishe mama mkwe akae,"

Wakimaliza kazi wana ndugu kibao walioonana nao siku moja tu.

**SWALI**

Mawe ya Matambawe yanapatikana sehemu gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Mke kanikimbia bila hata kugombana

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee kuelimishana kuhusu mikiki mikiki ya maisha. Mengi yamejificha katika familia zetu, huku mengine tukiyashuhudia na kudhani kuwa Maisha Ndivyo Yalivyo kumbe ni shida!

Tena ndoa nyingi hivi sasa zinaanza mitikisiko miaka ya mwanzoni tofauti ya miaka kadhaa iliyopita ambapo tafrani huanza baada ya miaka mitano kuendelea. Hapo wameshazaliwa watoto wawili au hata watatu, gari lipo na pengine ujenzi wa nyumba upo kwenye mchakato au tayari.

Wiki iliyopita tulimjadili kijana mmoja ambaye alioa binti ambaye hakuwahi kupata elimu kabisa. Akatamani sana kumuendeleza ili aweze kuendana na maisha yenye uelewa mpana kifikra.

Japokuwa alianza kumpatia mafunzo ya elimu ya msingi mwenyewe, alipotaka kumuinua zaidi kielimu binti akagoma. Pengine ni kutokana na kuona kwamba kwao wazazi hawakumsomesha na wapo wengi hawajasoma katika familia yao akajikatia tamaa.

Roho ya ujinga ama kwa hakika inatesa watu wengi, na ndilo lengo kuu la shetani kutesa wanadamu. Mungu anaweka bayana katika neno lake aliposema,

“Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa; kwa kuwa wewe umeyakataa maarifa, mimi nami nitakukataa wewe usiwe kuhani kwangu mimi; kwa kuwa umeisahau sheria ya Mungu wako, mimi nami nitasahau watoto wako”.(Hosea 4:6).

Ujinga ni mbaya sana na ni kifungo kikubwa kinachosababisha matatizo kwa wengi. Kiwango cha ujinga alicho nacho mtu, ndicho shetani hukitumia kumdanganya.

Nilieleza wiki moja iliyopita kwamba yupo mama alimvuruga mumewe kiasi cha kufikia hatua mume akaihama nyumba yake na kwenda kuanzisha maisha kwingine.

Baada ya muda kupita, mama akili ikarudi akagundua alipokosea, akaanza kuwatumia watoto kumshawishi baba yao arudi nyumbani. Baba akakataa kwani alishaanzisha maisha yake, akajenga nyumba na kununua gari lake lingine na zaidi ya yote anayo amani tele.

Msomaji wetu mmoja alipoisoma makala ile akanitumie ujumbe kuelezea naye jinsi mkewe alivyokimbia ndoa na kutokomea kusikojulikana. Akaona ujumbe hautoshi akanipigia kabisa simu. Akasema kwa tukio hilo yeye alishangaa kwani hawakuwahi kugombana na mkewe mbali na kuchakarika kimaisha kwa pamoja.

Akasema kwamba yeye ni mfanyabiashara na mkewe alikuwa tu mama wa nyumbani huku akimshirikisha kwenye biashara kadhaa kuongeza kipato cha familia. Walibahatika kupata mtoto mmoja.

Mtoto huyo akiwa katika umri wa miaka minne, mama akaanza vituko mara anachelewa kurudi nyumbani. Akiulizwa ananuna au anajibu kwa ukali. Ilibidi nivumilie kwani nilikuwa nampenda mke wangu sikutaka kumuudhi.

Siku moja nikitoka kwenye shughuli zangu kufika nyumbani nikaona tofauti. Mke wangu na mtoto hawapo na hata sanduku lake halipo. Kuuliza majirani wakasema hawajamuona akitoka.

Tokea siku hiyo sijamuona tena mke wangu na hata nilipofuatilia kwa ndugu zake hawakunipa habari zake. Ni miaka mitano tokea aondoke. Anamalizia kusema mpendwa huyu.

Msomaji wangu, vituko vya wanandoa kuzikimbia ndoa zao ni vingi. Na inakuwa mbaya zaidi mama anapoikimbia nyumba yake baada ya yeye kuwa chanzo cha anguko. Ni wazi kuwa mwanamke mpumbavu ndiye anayebomoa nyumba yake kwa mikono yake mwenyewe.

Niliwahi pia kueleza kwenye safu hii kwamba yupo mwanamke mmoja alichukuliwa kijijini na kuletwa mjini. Akaolewa na kijana mmoja aliyekuwa na kazi ya kuongoza watalii wanapokuwa katika ziara sehemu mbalimbali nchini.

Wakabahatika kupata mtoto mmoja. Baada ya miaka miwili bibie akabadilika akaanza kumwambia mumewe kuwa anahisi anaye mwanamke mwingine(hawara). Vinginevyo sharti aache kazi ili waishi. Mume akashangaa kwani kulikuwa hakuna kitu kama hicho. Na pia kwa nini aache kazi!

Mwanamke akaanza vituko, mara hali, mara hapiki, analala sebuleni. Siku moja narudi nyumbani nikakuta hayupo. Kumbe katoroka. Nikaenda kuripoti polisi.

Nikapiga simu kwao kijijini mama yake akanitukana kwamba nimemtesa binti yake na kwamba hatarudi tena kwangu. Nikabaki nashangaa.

Hata hivyo, nilizidi kufuatilia nikagundua alishaolewa na mtu mwingine. Cha ajabu aliishia kwenda kulima vibarua vya shamba kwa watu na mumewe mpya.

Mpenzi msomaji, wapo kinamama ambao sijui ni madudu gani huwaingia akilini na kutifukatifuka hadi kuchukua maamuzi yanayowapeleka kusiko. Hii ni roho ya ujinga inayopumbaza watu wengi inafanya kazi.

Wengi siyo wavumilivu katika ndoa na wanapokurupuka wanatengeneza majanga.

***Je, una kisa? Ujumbe 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi



# Tunahitaji saikolojia ya jinai kubaini mashoga, wasagaji?

KASHFA kuhusu baadhi ya Watanzania kujihusisha na mapenzi ya jinsia moja na kuweka hadharani haiba yao ni kama inaanza kuzoeleka na inatembea kwa kasi hasa kwa kundi la vijana ambalo ndilo tegemeo kwa shughuli za kiuchumi na uzalishaji.

Kama taifa, jambo hili tusipoweka nguvu kulidhibiti na kulichukia, litachukua miaka kadhaa, kukubali au kutokubaliana na hali hiyo. Hii ni kwa sababu inaonekana kuna mahali tulijisahau na kuacha mizizi kuota na uamuzi wa kupambana nalo unakwenda taratibu.

Najiuliza kwa yanayotajwa kuendelea nchini kuhusu ushoga na usagaji; Je tunahitaji msaada wa wataalamu wa ‘Forensic Psychology’, yaani uchunguzi wa kina wa saikolojia ya jinai kuwabaini wanaovuruga maadili yetu kama Watanzania au tuendelee kutumia sheria zile zile?

Kwa nini? Sababu ya kwanza ni kwamba forensic psychology pamoja na mambo mengine inashughulika pia na saikolojia ya uhalifu, ambao kwa maana nyingine ni utafiti wa mawazo na matendo ya wakosaji.

Kimsingi, forensic psychology inatoa jibu kwa swali la kwa nini wahalifu hufanya kile wanachofanya.

Kama ndivyo, ifike mahali ili kupamba na watu hawa kisawa sawa, ni lazima tutengeneze wanasaikolojia wa maisha halisi mitaani, kwenye maeneo ya starehe na maeneo ya huduma kama shule na kadhalika, ambao hawezi kuandamana na maofisa wa Polisi kukabiliana na washukiwa.

Hawa kwa kuzingatia ujuzi wao wa tabia ya binadamu, hasa kwenye eneo la jinai dhidi ya saikolojia ya uchunguzi, wanaweza kwa mfano, kuwasaidia maofisa wetu kutoa taarifa za wanaoendesha biashara ya mapenzi ya jinsia moja; na vilevile katika kuuliza maswali yanayofaa wakati wa kuhojiwa au kutoa mambo muhimu ili kusaidia uchunguzi wao.

Jambo baya zaidi, huko katika Jiji la Arusha kama tunaambiwa hali ni mbaya, kwa kuwa inakadiriwa vijana 4,000 wanajihusisha na mapenzi ya jinsia moja. Je mikoa mingine, hali ikoje? inawezekana ikawa ni zaidi ya Arusha.Ziko taarifa za kuaminika ambazo zinaeleza kuwa baadhi ya maeneo ambayo yanatajwa kushamiri kwa vitendo hivyo katika jiji hilo ni Vituo vya Makuzi ya Watoto (Day Care) na baadhi ya taasisi za kiraia (NGO) ambazo zinaomba usajili kwa minajili ya kutoa elimu kwa jamii.

Kwamba, kuna taasisi nyingine zinakuja kwa mgongo wa kutoa elimu kwa wananchi, kumbe zinakuja kuratibu masuala ya ushoga kupitia Day Care na katika vituo vya taasisi zao.

Niliwahi kuandika kataa utamaduni wa magharibi unazotweza utu, nikimaanisha vita inayoendelea sasa ya ushoga, usagaji ni masuala yanayochochewa na mabadiliko ya kijenetiki, ambayo huchochea tabia ya kutweza utu.

Ni kwa sababu, utu wa mwanadamu umegawanyika katika aina tatu za utu, yaani introvert, extrovert na ambivert.

Kwa ufupi sana, hili la mapenzi ya jinsia moja ndio haswa linaloguswa katika aina ya ambivert, ambayo inatumiwa sana na watu hawa tunaowakataa katika jamii kutokana na hulka yao na mienendo yao katika kuharibu taifa la Mungu.

Ni lazima Watanzania wajue kwamba, utu ni mchakato wa muda mrefu, ambao huanza na kuzaliwa na kuendelea katika utoto hadi ukubwani.

Kwa sababu, utu una jukumu muhimu sana katika tabia ya binadamu, tukatae tamaduni za magharibi zinazotweza utu!

Bunge letu kuagiza serikali, kufanya utafiti wa kina kuhusu ukubwa wa tatizo la ushoga au mapenzi ya jinsia moja hapa nchini, na mambo gani ambayo taifa linataka kwa wakati huu,

Yaongezeke kwenye Sheria ya Makosa yaKujamiana (SOSPA) ya Mwaka 1998 na Sheria ya Kanuni ya Adhabu (Penal Code), ni hatua kubwa katika vita hii.

Kwa sasa sheria zetu zinasema hata kukubali tu kuingiliwa kinyume na maumbile, ni kosa, na ni kinyume na kifungu 154 (1) (c) cha Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 ya Sheria iliyofanyiwa Marejeo ya Mwaka 2022.

Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. ***Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

## HARUSI



MAGAUNI YA TAUSI NI AINA YA NGUO ZINAZOPENDEZA KUVALIWA WAKATI WA SHEREHE YA 'KICHENI PATI' KUTOKANA NA MWONEKANO WAKE MZURI.

# MITINDO
## Na Moshi Lusonzo

# MAXI HAINAGA TATIZO

GAUNI aina ya Maxi ni vazi la kale, lakini kutokana na mwonekano wake usiopitwa na wakati limekuwa likipendwa na wanawake wengi.

Kimsingi gauni la Maxi limebuniwa kulingana na mtazamo wa kulia hasa unaozingatia heshima, maadili na mtazamo.

Nguo ya aina hii, inampa mvaaji kuwa na mwonekano mpana zaidi na uhuru wakati wote anapotembea au kukutana na watu mbalimbali.

Muundo wa gauni hili lenye urefu wa kwenda chini, pana na rangi ya kuvutia ni nzuri kuvaliwa na kila mwanamke mstaarabu na anayependa stara.

Jambo la muhimu kabla ya kununua ni lazima kuchunguza na kujihakikishia kama kitambaa chake ni imara na bora na mzunguko wake unatosha kukupa nafasi.

Sio kwamba ni kanuni au sheria, lakini jambo zuri kama unapenda kuongeza na koti au shati juu kama itakupatia hewa ya kutosha.


Kama una urefu wa kadiri basi unashauriwa kuvaa viatu virefu ili kukuwezesha kuwa na muonekano bomba. Endapo una urefu wa kutosha ni vyema ukachagua viatu vifupi ili kupunguza urefu wako.





UREMBO

Na Mary Geofrey



# RUDISHA UREMBO

## Kunywa juisi ya Tende na Maziwa

JUISI ya tende na maziwa imezoeleka kutumiwa kama kifungua kinywa nyakati za asubuhi au jioni pale watu waliofunga.


Hata hivyo, katika suala la urembo kinywaji hiki kinaaminika kuwa na uwezo wa kuongeza mvuto wa mwili na kuupa mwili nguvu.

Tende na maziwa inaaminika kuwa na vitamin C ambayo husaidia kufanya ngozi iwe na unyevu lakini pia iwe laini.

Maziwa yana vitamin B12 ambayo husaidia katika kufanya ngozi ipate mng'ao na kutibu chunusi na madoa.

Kusaidia kukinga ngozi na mikunjo

Maziwa yana Vitamin D ambayo husaidia katika kuondoa mikunjo ya ngozi, kufanya ngozi yako ionekane kijana zaidi pia tende husaidia katika kufanya ngozi ipate afya na kuondoa mikunjo.



**Nywele imara**

Tende zina virutubisho ambavyo husaidia kufanya nywele zako ziwe kakamavu wakati maziwa yenyewe yanasaidia kuleta mng'ao katika nywele zako.

Kufanya Nywele Ziwe Na Afya

Tende zina vitamin B ambayo husaidia kuzipa nywele afya.



MAPISHI

Na Mary Geofrey

# JUISI YA UKWAJU

UKWAJU ni aina ya kichangamsha mdomo ambacho unaweza kula kama ilivyo au kutengeneza juisi.

Wengi hawapendi kula kwa kumumunya kwa sababu ya uchachu wake na ndio sababu ya kutengeneza juisi.

Katika safu yetu ya mapishi wiki hii tutaelekezana namna ya kutengeneza juisi ya ukwaju na faida zake.

**Mahitaji**

Ukwaju, Sukari, Limao na Vanilla.

**Jinsi ya kuandaa**

Chukua ukwaju, usafishe kidogo na tia katika sufuria, weka maji kiasi kisha chemsha kwa muda wa dakika 10 hadi 20.

Baada ya hapo anza kuchemsha ukishakuwa tayari uepue na uache upoe.

Ukishapoa chukua chombo kisafi na maji safi kisha anza kuchuja juisi yako vizuri.

Kisha ichukue na kuongeza ladha kama unga wa vanillah na sukari kiasi upendacho kisha koroga vzr kisha iweke katika jokofu ipoe tayari kwa matumizi.

**Faida ya juisi**

Faida ya kwanza ni kusaidia mmeng'enyo wa chakula na huondoa hali ya kuvimbiwa na sumu mwilini.

Huzalisha antioxidants ambayo huzuia tatizo la saratani.

Inaongeza vitamini B na C pia Carpenters hushusha joto la homa ya Maleria na ya tumboni hulinda mwilini na kukuondolea kero za mafuta ya kooni.



MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Epuka nyumba yako kutitia baada ya muda mfupi kwa kufanya haya

KAMA ilivyo kwa viumbe hai kuathiriwa na mazingira wanayoishi, ndivyo ilivyo pia kwa viumbe visivyo hai ikiwamo nyumba.

Ili kuepuka majengo yasiathirike, ni vema ubunifu wake ufanyike katika hali ya ubora wa hali ya juu katika sehemu husika linapojengwa jengo.

Msanifu majengo, Deodatus Charles, anasema hata ujenge nyumba nzuri na kubwa kiasi gani, kama haijabuniwa na kujengwa kwa kuzingatia mazingira ya eneo husika, lazima iwe hatarini kuathirika.

Anasema kabla ya kuanza kujenga nyumba ni lazima ufanye uchunguzi katika eneo husika kubaini endapo kuna magonjwa yanayoweza kuathiri nyumba yako na kufanya ubunifu wa kukabiliana nayo.

Mtaalam huyo anasema endapo nyumba hiyo itajengwa pasipokufanyiwa ubunifu mzuri huenda ikaathiriwa na magonjwa hayo.

Anasema miongoni mwa magonjwa yanayoathiri nyumba endapo haijafanyiwa ubunifu mzuri ni kutitia.

Kwamba mara nyingi hutitia kutokana na aina tofauti za udongo,



kiwanja au kimo cha msawazo wa msingi kuwa tofauti pamoja na ubunifu hafifu wa udongo kulingana na uzito wa jengo husika.

Ugonjwa mwingine anasema ni nyumba kupitisha maji, na kwamba maeneo mengi ya Tanzania yamezungukwa na vyanzo vya maji ambayo yanahitaji usanifu na ubunifu wa hali ya juu wakati wa ujenzi wa nyumba ili kuepuka athari baadae.

"Maeneo mengi ya pwani majengo yake mengi yameathiriwa na tatizo hili na hata limekuwa kero kwa wakazi na watumiaji wa majengo hayo. Baadhi ya majengo yanapitisha maji kwa njia ya sakafu na kuta mithili ya chujio au chemchemu na mara nyingi utagundua kwa kuona ardhi yake inatoa maji wakati wote wa majira ya mwaka."

" Na majengo mengi ya maeneo haya yanaoza na kutitia kwa haraka na hata mashimo ya vyoo vyake huinuka kwenda juu ambalo ni hatari kwa afya za wakazi. Katika hali hii kuta na sakafu huoza kwa haraka kutokana na maji yaliyopo chini ya ardhi kuwa na kemikali mbalimbali zilizopo kwenye maji hayo. Kwa hiyo katika mazingira haya lazima yatumike malighafi sahihi za kuzuia maji hasa wakati wa ujenzi."

Jingine anasema ni kuoza kwa nyumba na kwamba hali hiyo hutokana na unyevunyevu na kemikali mbalimbali kupitia maji kukaa kwa muda mrefu kwenye kuta na kuathiri ubora wa kuta hizo.

"Na hii husababisha kumea kwa mimea ambayo kusababisha ukungu wa kijani kwenye kuta ambao huzalisha fangasi mbalimbali wanaokula kuta.".

## Namna rangi inavyoongeza afya

**Na Restuta James**

PAMOJA na kwamba rangi inayoshika namba moja kwa ajili ya nyumba ni bluu tulivu, uwanja wa mapambo ya ndani una mapendekezo rangi lukuki kwa ajili ya vyumba na sehemu za mapumziko.

Aidha, rangi hizi zimegawanywa katika namna ya ajabu, kiasi kwamba inatuhitaji muda zaidi kuzitambulisha kwako msomaji wa ukurasa huu.

Wataalamu wa mapambo ya ndani wamezigawa kwa kuzingatia pande nne za kaskazini, kusini, magharibi na mashariki pamoja na mwelekeo wa jua wa chumba husika. Rangi za kuta hizi nne nitakuletea wiki ijayo kwa kuwa leo ninakupitisha kwenye rangi zenye utulivu unazoshauriwa kupaka kwenye chumba cha kulala.


Bila kuisahau bluu tulivu niliyoitaja hapo juu, rangi ya beige inatajwa kuwa na utulivu na kumfanya mtu apate usingizi mwororo na kuamka mwenye nguvu ya kutosha.

Wanaeleza kuwa ni rangi yenye athari chanya kwenye mfumo wa neva na hivyo ili kuboresha afya yako, unahitaji kupanga vizuri chumba cha kulala kwa kuzingatia rangi zitakazokupa utulivu kutokana na kazi za mchana kutwa.


Kwa mujibu wa wataalamu wa mapambo, rangi nyingine ni kijivu. Hata hivyo, wanashauri kwamba ili kupata utulivu na matokeo mazuri kwa ajili ya kupumzisha akili, rangi hii ipakwe na nyeupe au bluu tulivu.

Kwenye orodha hiyo, rangi ya machungwa (baby orange), inatajwa kuwa na matokeo mazuri ikiwa 'itatupiwa' kwenye chumba cha kulala. Inashauriwa kwamba rangi hii isipakwe kwenye ukuta mkubwa. Unaweza kuipaka kwenye meza yako ya kujipambia (dressing table) au kipande kidogo cha ukuta utakacho kichagua.

Rangi nyeupe haijasahaulika kwani yenyewe inaweza kupakwa kwenye chumba bila rangi nyingine au kwa kuchanganya pia.



## KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
GARI ILIPOSIMAMA KUCHIMBA DAWA NA WATU KUPATA CHOCHOTE UKAVAMIA 'KITI KIREFU' ALAFU UPO SAFARINI ULITEMEGEA NINI?
DEREVA UCHAFUZI WA MAPORI ILIKUWA ZAMANI ASIKULAZIMISHE UPAKI KARIBU NA VICHAKA
ALIVYOZIKUMBATIA NA KUZIFAKAMIA NILIDHANI ANA CHOO CHAKE BINAFSI
JAMANI MWENZENU 'NITAPUU' HUMU HUMU!
PUU' UONE! KWANI SISI SIO WALEVI MBONA TUMEZIKAUSHIA
HUYO ALITAKA TUMJUE KAMA ANAZO KWA NAMNA ALIVYOAGIZA KWA NYODO HAKUJUA KAMA ZITASHUKA HA HA HAAAA ATAJIBEBA!
NASEMA AJIKAZE NIKIANZA KUSIKIA HARUFU TU, NNAE!
TOKA NITIMULIWE KAZI NAONA POMBE ZA KIENYEJI ZINAVAIBU KWANGU KULIKO BIA SIJUI KWANINI!
'USISHANGAE UMEPOKELEWA VYEMA NA MIZIMU' JIANDAE KUNYONYOKA NYWELE
MKE WANGU TUMEPANGA CHUMBA AU KIVULI CHA MTI?
MASWALI HAYO KAMUULIZE DALALI ALIYEKULA HELA YAKO
SIKUKUU YOTE TUMEKULA CHALINZE NA MWANANGU ILA INGINE TUTAKUWA NA WEWE
BABA! ULIAHIRISHA TUKAENDA KULALA MBAGALA KWA ANTI FETY SAKABONA
JITETEE HAPA HAPA, YULE MZEE ALIKUKATAZA ULIPONIOA USITHUBUTU HATA KUNIFINYA! LEO NAMPELEKEA KESI YA KUNIKABA KABALI
INAMAANA 'WAIF' KUKUPITISHA NJIA ZENYE MABANDA YA CHIPSI ULIDHANI SIJUI NJIA ZA MKATO KUFIKA HUKU?
UKWENI
NILIPOSEMA "MIMI NI MTU MKUBWA" SIKUMAANISHA NI MHISHIMIWA SEREKALINI ILA NI SAWA NA BABAAKO
BABA YANGU ALIKUWA ANAITWA 'PEPEKALE' JE, NA WEWE EMOLO AU BILEKUMPASI?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
SHEMEJI NI MUME WA DADA YAKO KUWA MPOLE...

## HABARI KIMATAIFA

# Kiongozi RSF aapa kupigana, adai anailinda nchi ya Sudan

**KHARTOUM,** SUDAN
MMOJA wa majenerali wawili , wanaoongoza kikosi cha dharura (RSF) kinachopigana dhidi ya jeshi la Sudan, amesema hatafanya mazungumzo mpaka mapigano yaishe.

Jenerali Mohamed Hamdan Dagalo, anayefahamika zaidi kama Hemedti, alisema hivi karibuni kuwa wapiganaji wake wanapigwa na mabomu tangu mkataba wa siku tatu wa kusitisha mapigano uongezwe.

"Hatutaki kuiangamiza Sudan," alisema jenerali huyo na akimlaumu mkuu wa majeshi Jenerali Abdel Fattah al-Burhan, kwa kuongeza ghasia.

Jenerali Burhan amekubali kufanya mazungumzo ya ana kwa ana nchini Sudan Kusini.

Urefushaji wa muda wa usitishaji mapigano ulifikiwa Alhamisi usiku kufuatia juhudi kubwa za kidiplomasia za nchi jirani, pamoja na Marekani, Uingereza na Umoja wa Mataifa.

Akizungumza na BBC kwa njia ya simu, Hemedti alisema kuwa yuko tayari kwa mazungumzo lakini kwa sharti kwamba usitishwaji wa mapigano unaheshimiwa.

"Acha uhasama, baada ya hapo tunaweza kuwa na mazungumzo." alisema

Alisema kuwa hana tatizo la kibinafsi na Jenerali, lakini anamchukulia kama msaliti kwa kuwaleta ndani ya serikali wale waliokuwa watiifu kwa rais wa zamani Omar al-Bashir, ambaye alipinduliwa na jeshi na RSF kwa pamoja mwaka 2019.

Utawala wa Bashir ambao ulikaa madarakani kwa miongo mitatu, ulifahamika kwa itikadi zake kali za Kiislamu na kuweka masharti makali ya sharia.

"Kwa bahati mbaya Burhan anaongozwa na Waislamu viongozi wenye itikadi kali," Hemedti alisisitiza

Mnamo 2021, yeye na Jenerali Burhan walikataa makubaliano ya kugawana madaraka na raia, na kuchukua udhibiti kamili wa mapinduzi.

Walikosana mwaka huu kuhusu pendekezo la kurejesha mamlaka ya uongozi wa kiraia, hususan muda wa kuwajumuisha wanajeshi wa kikosi imara cha Hemedti cha wanajeshi 100,000, wanaounda kundi la Rapid Support Force's (RSF) ndani ya jeshi.

"Ninatamani kuwa na serikali ya kiraia leo, serikali kamili ya kiraia. Huu ndio msimamo wangu ," aliongeza Hemedti wakati akizungumza na BBC.

Hemedti alisema wapiganaji wa RSF sio maadui wa wanajeshi , bali wanalinda nchi hiyo dhidi ya mabaki ya serikali ya miaka 30 iliyopita.

"Hatutapigana na nyinyi. Tafadhali nendeni kwenye vitengo vyenu vya kijeshi na hatutapigana nanyi ." aliongeza.

Kauli hiyo ya Hemedti imeleta hofu kwa mamilioni ya watu ambao wanaendelea kukwama kutoka mji mkuu Khartoum, ambako kuna uhaba wa chakula, maji na mafuta.

**BBC**



Wingu la moshi likitanda angani wakati mashambulizi ya pande mbili za jeshi nchini Sudan zinazohasimiana kuendelea na mapambano ya kuchukua madaraka. **PICHA: DW**

## Brazil kutenga maeneo ya wazawa

**BRASILIA,** BRAZIL
Rais wa Brazil Luiz Inácio Lula da Silva, ametia saini amri ya kuanzisha maeneo zaidi yaliyohifadhiwa kwa ajili ya jamii za wazawa kwenye taifa hilo la Amerika ya Kusini

Uamuzi huo ambao ni kwanza kufanyika tangu mwaka 2018 , unalenga kutenga maeneo mapya sita ya jamii za wazawa ambao wengi bado wanaishi kwenye vijiji vilivyo misituni.

Akionesha dhamira ya kutimiza ahadi yake ya kuzuia ukataji wa miti na uharibifu mkubwa wa mazingira hususani kwenye msitu wa Amazon.

Rais Lula alisema ataendelea kutenga ardhi kwa ajili ya jamii za asili, zinazosifika kwa utunzaji mkubwa wa mazingria.

Mwanasiasa huyo wa mrengo wa kushoto anataka ifakapo mwaka 2030 kusiwe na shughuli zozote za ukataji wa miti ndani ya msitu wa Amazon, unaotegemewa na Ikolojia ya dunia.

**DW**

## Ukraine yaomba msaada zaidi

**KYIV,** UKRAINE
Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensk, amewarai washirika wake kuipatia nchi yake mifumo ya kisasa ya ulinzi wa anga ikiwemo ndege za kivita, baada ya mashambulizi ya Russia kuhujumu maeneo ya makazi ya watu.

Akizungumza kupitia ujumbe wa kila siku kwa njia ya video, Zelensky alisema bila anga iliyo salama ulinzi wa taifa hilo utaendelea kuwa mashakani na amewatolea mwito nchi washirika kuipatia nchi hiyo mifumo na zana zinazohitajika.

Kiongozi huyo amelaani vikali mashambulizi dhidi ya mji wa Uman ambayo yamesababisha vifo vya watu 23, wakiwemo watoto watatu na kuituhumu Russia kuhusika na hujuma hiyo.

Zelensky amesema HYPERLINK "https://www.dw.com/sw/mashambulizi-ya-urusi-yawaua-12-ukraine/a-65460904" ukatili wa Urusi unaweza kuzuiwa kwa kutumia silaha kama wanavyofanya wanajeshi wa Ukraine lakini vilevile kupitia vikwazo vikali vya kiuchumi kutoka Jumuiya ya Kimataifa.

**DW**

## Papa Francis aonya Ulaya kukumbatia vita

**BUDAPEST,** HUNGARY
Kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis anaendelea na ziara nchini Hungary, na kuzitaka nchi za Ulaya kuacha alichokiita 'ugomvi wa kitoto' na kukumbatia maadili ya waasisi.

Hotuba hiyo ya kwanza ya Papa Francis katika ziara yake ya siku tatu nchini humo, ilitolewa mbele ya Waziri Mkuu Viktor Orban na viongozi wengine wa ngazi za juu. Papa Francis alisema Ulaya inapaswa kurejea katika mitazamo ya waasisi wake, ya kujenga diplomasia yenye uwezo wa kuunganisha watu, badala ya kupanua migawanyiko. Ameonya dhidi ya mwamko wa kivita kuzidi nguvu ukomavu uliofikiwa baada ya madhila ya vita, na kuruhusu hatua za kurudi nyuma katika hali ambayo ni sawa na ugomvi.

"Ni kama vile tunashuhudia kutoweka kwa ndoto ya amani, na nafasi yake ikichukuliwa na wanaopiga ngoma ya vita," alisema kiongozi huyo wa kidini.

Aliongeza kuwa azma ya kujenga amani na utengamano wa jumuiya ya kimataifa inayumba, kanda za ushawishi zinaundwa, tofauti zinatiliwa mkazo, utaifa unaimarika na lugha kali ya makabiliano inapaza sauti.

Papa Francis na Waziri Mkuu wa Hungary, Viktor Orban wana maoni sawa katika kuhimiza mazungumzo kama juhudi ya kumaliza vita vya Ukraine, lakini wanatofautiana juu ya suala la wahamiaji.

Orban ni mfuasi wa sera kali ya kupinga wahamiaji kama njia ya kulinda Ukristo ndani ya Ulaya, wakati Papa Francis akitaka wale wanaokimbia vita na umasikini wakaribishwe.

**DW**

## MAKALA

# WEMA SI KINGA YA UHALIFU



Na Magabilo Masambu

KUNA dhana imejengeka miaka mingi katika jamii hasa za kiafrika kwamba yeyote anayetoa misaada kwenye jamii anatafsiriwa kuwa ni mtu mzuri na kwamba hawezi kuwa mkosaji.

Kutokana na dhana hii, wakati mwingine hata wale wanaotusaidia wanapotenda makosa ya waziwazi inakuwa ngumu kuwaambia makosa yao maana tutakosa misaada.

Lakini upande wa pili wale wanaotenda uhalifu mkubwa na mdogo nao wanatambua nguvu ya kusaidia ili wanapoonekana wametenda maovu, iwe kazi ngumu sana kuwatia hatiani.

Wakati mwingine hali ya umasikini inachangia kuogopa kumsema mtu kwamba anatenda maovu hata kama maovu yake yanajulikana.

Pale Mtibwa Turiani, Morogoro miaka ya 1990 wenyeji watakumbuka, amewahi kutokea jamaa fulani aliyetingisha wakazi wa eneo hilo na viunga vyake.

Jamaa yule alikuwa anaendesha mauaji ya watu mbalimbali, alikuwa anajificha kwenye miwa au msituni akivamia watu na kuchukua vitu walivyokuwa navyo, kisha ama kuvItupa na vikaokotwa na watu au kuwapatia watu aliokuwa akiwafahamu.

Serikali ilimtia nguvuni na kumfunga miaka kadhaa. Pamoja na yote hayo, kuna baadhi ya watu bado waliendelea kuamini kwamba kwa roho nzuri yake ile alisingiziwa hakuwa anatenda.

Mwaka 1995, kule Kibara, Bunda hasa katika vijiji vya Bulenda Bufwe, Kibara, Nyakatubha, Nyamuhula na Mwigundu, kuliibuka kundi la watu waliokuwa wanakaba watu usiku na jambo lisilokuwa la kawaida ni kwamba ukinigwa (kukabwa shingoni) ukapiga kelele.

Watu wa jirani yako walikuwa hawasikii zile kelele, walikuwa wanazisikia watu wa kijiji cha pili na mara nyingi walikuwa wakikuniga ukiwa gizani kwa hiyo hakuna anayeona kama umekabwa.

Jambo hili lilifanya nyakati za usiku tulale nje, maana hawakuwa wananiga mchana bali ni usiku tu tena kukiwa hakuna mwanga tukawa tunawaita "Abhanyigi" watu wa maeneo hayo watakumbuka kisa hiki.

Kibaya zaidi, wakati huo palikuwa na njaa kali sana na walichokuwa wanafanya hao wanigaji, walikukaba hivyo ujisaidie kisha wanachukua kinyesi chako wanachanganya kwenye unga. Kwa hiyo kama ni njaa mfe maana mtakwenda kumwaga huo unga.

Baadhi yao baadaye walikuja kubainika maana hakuna kitu utafanya nyakati zote kisijulikane hata kama ni cha siri kiasi gani. Utafanya kwa muda tu ndiyo maana kuna msemo wa za mwizi ni 40.

Baada ya kujulikana kwamba ndiyo wanafanya mchezo huo na kwenye jamii ni watu wanajulikana kwa wema.

Bado walipata watetezi wengi waliokuwa wanasema hawa watu wanatusaidia sana, hawawezi kuwa wametenda hayo. Serikali ilipofanya uchunguzi ikabaini ni wao, wakachukuliwa na baada ya hapo hatukuona tena visa hivyo.

Turudi kwenye familia zetu, matendo maovu yote mara nyingi huanzia nyumbani. Hakuna mwizi anaanza kuiba kwa jirani bila kwanza kuiba kwao.

Kinachotokea ni kwamba, huyu mwizi wa nyumbani huwa anaonyesha unyenyekevu wa hali ya juu nyumbani kiasi cha kutetewa anapoanza kutenda uhalifu kwa majirani.

Mama zetu wamekuwa wakiingia kwenye mtego huu zaidi, mashtaka yakiletwa nyumbani, mama anakuwa wa kwanza kusema mtoto wangu hawezi kufanya hivyo na wakati mwingine kama baba hayupo hatajua kilichotokea, kidogo kidogo tabia inakua mwisho mtoto anakuwa jambazi.

Dunia hii ina watu wanatenda mambo mabaya sana yasioonekana lakini ni hao hao wako mstari wa mbele kutoa misaada kwa wahitaji na inapojulikana kwamba ni waovu, wanaopata misaada wanakuwa wa kwanza kuwatetea si kwa sababu hawatendi maovu, bali hoja hapa inakuwa wanasaidia sana jamii.

Kusaidia watu hakuzuii mtu kuwa mhalifu. Hata majambazi wanaiba wanaleta sadaka kanisani.

Ushauri wangu kwa jamii, pamoja na kwamba tunazo shida nyingi sana za kimaisha.

Kuna umuhimu wa kuwa makini sana na wale wanaohitaji kutusaidia, si kila msaada ni msaada. misaada mingine inaandaa maangamizi yako bila wewe kutambua.

Sisemi kwamba tusisaidiwe lakini ni muhimu kujua maana ya misaada hiyo.

Kwa baadhi ya nchi za Ulaya ambazo nyingi zinatupatia misaada hapa, kwao huko ukimpatia mtu hata ofa ya chakula tu anaweza kukushitaki, kwasababu anaamini huwezi kumapatia ofa bila kuhitaji kitu kutoka kwake au wakati mwingine naona umemdharau.

Zamani tulikuwa tukiogopa wanyama wakali wa mwituni lakini siku hizi binadamu ni mnyama wa kuogopa kuliko mnyama yoyote unayemjua.

Fedha imekuwa na nguvu zaidi kuliko utu. Siku hizi mtu akikupa lifti kwenye gari na hamfahamiani ukafika salama, mshukuru Mungu wa Mbinguni na usikubali lifti ukiwa peke yako.

Siko hapa kutaka kumuhukumu mtu lakini itoshe kusema kwamba, yanaoendelea huko Kenya kwa sasa, yatufungue machao kama taifa ili kuona.

Tusiwe makondoo yanayopelekwa machinjioni, tuwe watu wa kudadisi ili kuujua ukweli kabla ya kufanya uamuzi wa jambo lolote.

Tofauti ya mbuzi na binadamu ni utashi.

Usipotumia utashi katika kuamua mambo, maana yeke wewe ni mbuzi uliyevaa mwili wa binadamu, hivyo ni rahisi kupelekwa machinjioni.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Dar es salaam-Tanzania**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Dunia uwanja wa fujo, mwenye ngoma zake acheze zipasuke



Na Adam Fungamwango

TANGU karne na karne, wahenga, wakiwemo wanamuziki, watunzi na washairi, utenzi na insha waliisimulia dunia jinsi ilivyo na mambo yake. Wapo waliosema dunia siyo mbaya, ila walimwengu ndiyo wabaya. Kuna waliosema dunia ni tambara bovu. Yupo aliyesema dunia rangi rangire, yaani ni nzuri kuitazama ikipambwa na rangi mbalimbali, lakini wakati mwingine sivyo ilivyo.

TX Moshi William akiwa na bendi ya Polisi Jazz, aliwahi kutunga wimbo akauita 'Dunia.' Maudhui ya wimbo huo anauliza nyota na mwezi usiku vinag'ara, bili yake analipa nani? Akamalizia kusema dunia ni watu na si ardhi.

Ukiangalia hapa utagundua kuwa dunia ni kama uwanja tu au jukwaa, ambamo ndani yake mna watu, au binadamu na viumbe vingine.

Hata hivyo, binadamu ndiyo anatawala viumbe vyote na hapa duniani ndiye mwenye matatizo zaidi kuliko kiumbe yoyote yule.

Tembo, Simba, nyati, kirafu, nyangumi na wanyama wote wakubwa pamoja na nguvu walizokuwa nazo, lakini hawafui dafu kwa binadamu.

Binadamu ni kimbe dhaifu sana kwenye mauala ya nguvu kuliko wanyama wengi, lakini amepewa akili nyingi na ndizo anazotumia kuwatawala viumbe wote duniani.

Nani aliyempa akili biandamu? Ukirudia maandiko ya dini zote ni Mwenwezi Mungu na akamfanya kuwa mfalme wa dunia kwenda kuwatawala wanyama wote wa majini na ardhini.

Ni yule yule ambaye Tx Moshi aliuliza mwezi na nyota vinaangazia watu duniani usiku wakati giza limeingia, bili yake analipa nani?

Mungu alimbariki binadamu na kumpa uwezo wa ajabu, ndiyo maana si tu akawa anaitawala dunia, bali kutengeneza vitu mbalimbali kama maghorofa, ndege, treni, meli, manowari, magari, simu za mkononi, kompyuta na vingine vingi ambavyo tunaweza kujaza kurasa zote hapa.

Kwa bahati mbaya ni kwamba baadhi baadhi yao walipewa uwezo, badala ya kuleta maendeleo duniani wao wakaleta shari.

Popote kwenye mkusanyiko wa watu na hata wanyama ni lazima kuwe na kiongozi. Kwa binadamu kuna baadhi ya watu waliopewa uongozi wakaifanya dunia kuwa si sehemu salama ya kuishi miaka hiyo ya nyuma iliyopita.

Hata sasa, kuna baadhi ya nchi zinapata viongozi ambao badala ya kuongoza watu nchi ikaendelea, wao wanaleta matabaka, kuleta umwamba, kulipiza visasi na wakati mwingine kufanya mauaji, wakijiona wao ni bora sana kuliko wengine.

Binadamu wa aina hii wapo sehemu mbalimbali, hata mitaani tunapoishi, makazini, kwenye makampuni, mashirika, kuna viongozi ambao wanakuwa ni marafiki kwa wafanyakazi wao, lakini wengine wanataka wao waonekane kama 'muingu watu.'

Ndiyo maana wale wanaoteseka na utawala na mabavu wanabaki tu kusema kichinichini, "fanya yote, lakini ukumbuke wewe siyo Mungu, ni binadamu tu kama sisi, uliumbwa kwa udongo, utarudi kwa udongo, umwamba wote lakini kwa Mungu ni bure tu."

Baadhi ya binadamu wana tabia ya kujisahau wanapopata madaraka wanaanza kutesa wenzao na kuwadhalilisha kama si watu, hii ni mbaya sana kwa sababu kiongozi na wote wanaotawaliwa ni viumbe vya Mwenyezi Mungu na kwake wote ni sawa tu.

Ukitaka ujue hili ni kwamba, kiongozi ambaye analindwa na anapata matibabu ya hali ya juu, anafariki, lakini mwananchi wa kawaida ambaye hata dawa kutuliza maumivu anakosa yeye anabaki hai. Kama lingesimamiwa na binadamu, watu wa chini wangeanza kufa kabla ya matajiri na viongozi. Wote wanazikwa ardhini, masikini, tajiri, mwananchi wa kawaida na kiongozi, wote wanafukiwa chini. Mungu pia anatoa hewa ya 'oxygen' bure yeye mwenyewe, kila kiumbe kinavuta. Kama hili lingekabidhiwa kwa binadamu, nadhani saa hizi duani hapa watu wangeanza kulipishwa kama vocha.

Marehemu Marijani Rajab aliliona hili kwenye miaka ya 1980, akaja na kibao alichokiita 'Dunia Uwanja wa Fujo.' Kila kila kitu kuhusu hili.

"Ndugu yangu tizama unakoktoka. Hii dunia uwanja wa fujo mwenye ngoma zake acheze zipasuke, imewashinda wahenga wenye ujuzi, wametoweka na kuiacha vile vile. Inafaa kwenda nayo polepole, haitaki kujiweka kifua mbele.

Usijinate na kujiona mzuri, ubinaadamu hujafa hujaumbika. Hicho cheo ulichonacho ni dhamana, usisahau mpanda ngazi hushuka.

Usiwatese binadamu wenzio, aliwanyima ndiye yeye aliyekupa. Hao makatili yalioitikisa dunia, wako wapo mbona nao wametoweka?

Shauri yako lololo, wacha niimbe mwana wa Rajabu baba. Ninakueleza ukweli kaka. Sikia mambo. Na kama huitambui tambua. Bwana Mungu kaumba dunia, kamuumba Adam na Eva, ndiyo maana twaitwa Wanaadamu, mwanadamu kapewa uwezo wa kufanya kile anachotaka, wengine walipewa uwezo mpaka wakakufuru Mungu. Tulisikia hadithi za zamani alikuwako Firauni, yeye alipewa uwezo mpaka akajiita Mungu, katengeneza pepo yake na moto, akafanya madhambi kila aina, lakini jiulize yuko wapi?"

"Mwingine Mjerumani mmoja, kwajina anaitwa Hitler, alitaka atawale ulimwengu, mamilioni ya watu kachoma moto, wengine kapasua matumbo, wengine kawataka vichwa, lakini julize yuko wapi? Juzi juzi mwendawazimu mmoja, si mwingine Nduli Idd Amin, kaua ndugu zetu bila sababu, ati na yeye alijigamba, kwamba yeye hatishwi na lolote, tumempiga pigo takatifu mpaka kaikimbia Uganda, vile vile na yeye kashindwa."

"Sasa wewe ndugu yangu nini, dunia umeikuta, nawewe utaiacha, ubaya utakusaidia nini? Kula ugali wako wakalale." Anamaliza mwana wa Rajabu. Upo hapo?

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

MIEZI miwili tu baada ya ndoa, Husna anapigiwa simu ya mtu asiyemfahamu. Haikuwa simu ya heri. Ni simu ya mtu anayeonekana amedhamiria. Amedhamiria kufanya kitu alichokikusudia. Kwenye maisha ya ndoa aliambiwa yatakuwa ya shida na raha, lakini kwake haikuwa mapema kiasi hicho. Alihisi sasa hakuingia kwenye ndoa aliyoikusudia bali ni ndoa ndoana.Ni nani aliyempigia simu Husna? Alitaka nini? Lengo lake hasa ni nini? Ni kweli alichokusudia mpiga simu ndicho alichokihitaji ili kuvuruga ndoa hiyo? Nenda hatua moja moja kwa kusoma kila nakala ya toleo la Nipashe ili upate ukweli mzima wa kisa hiki cha utata, kusisimua, kusikitisha na chenye mafunzo makubwa kwa jamii na wanandoa wote.

# Simu ya Sumu-8

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

HIVI mfano wewe ndiye ungepigiwa siku na mwanaume wangu mimi akakuchamba kama alivyofanya huyo wako, ungenisamehe?"

Akauliza swali la ghafla na gumu. Dan akabaki kimya, hakujibu kitu, akabaki kumkodolea macho mkewe.

"Ni wazi ungeniacha." Akasaidiwa kujibu na muuliza swali.

"Basi inatosha mwanangu, ingia ndani, usipoteze nguvu zako bure kwa mwanaume kama huyu." Ilikuwa ni sauti ya Tabia, mama mdogo wa Husna ambaye muda mrefu alikuwa mlangoni akisikiliza kilichokuwa kikiendelea baina ya wanandoa hao.

"Mama hata wewe? Mi nilidhani ulipaswa kutusuluhisha, unazidi kuchochea moto!"

"Nini? Yaani umetoka huko uje kumbembeleza tena mwanangu akukubalie arudi tena jehanamu, ukamkutane na mahawara zako!"

"Mama, nyumbani kwangu unapaita jehanamu?"

"Ndiyo, tena zaidi ya jehanamu, angalia mwanangu alipoka hapa na hivi sasa alivyo. Ulimkuta japo na shida zake, ananisaidia kuuza mama lishe, lakini alikuwa mzuri mrembo, leo hii yupo hivi.

Ulimchukua na afya yake nzuri, umekwenda kumfubaza mwanangu umepauka kama kitande cha muhogo. Hivi Husna mwanangu unajiona ulivyofubaa?" Akamgeukia binti yake.

"Miezi miwili tu tangu uolewe uko hivi ukikaa mwaka je, si utakuwa kama bibi kizee cha miaka 80!" Tabia alizidi kuponda. Akageuka na kumtazama tena mkwewe Dan. "Hapa mwanangu hatoki."

Dan alijiona ni mtu mwenye mkosi kuliko yoyote aliyewahi kugusa sayari hii ya dunia. Aliona dunia haimtaki. Amekuwa mtu wa kukosana na kila mtu. Kwanza amegombana na mkewe. Halafu akaenda kulaumiwa na ndugu zake. Akaenda kukutana na moto wa Ziada. Akarudi tena kwa mkewe Husna akakutana na moto mkubwa kushinda wa kwanza. Mama mkwe naye akaongeza petroli kwenye moto unaowaka.

*********************************

Wingu kubwa jeusi lilitanda kwenye jiji la Dar es Salaam. Lilionekana kuwa na hasira kubwa na kulinyima nafasi jua kufanya kazi yake ya kila siku.

Siku hiyo lilionekana kabisa kutaka ufalme hata kwa siku moja. Jua kila lilipofurukuta lililosa kabisa nafasi ya miale yake kupiga kwenye jiji hilo.




**Mtu yule alikuwa akipiga hatua moja baada ya nyingine kuelekea anakoelekea. Mtu mwingine alikuwa nyumbani kwake. Alikuwa amepigiwa simu kuwa atafika nyumbani jioni siku hiyo. Na kwa sababu siku hiyo hakuwa na kazi nyingi na mizunguko pia, alirejea nyumbani mapema kumsubiri mgeni wake.**

Hali ikawa tofauti na siku zote. Dar ambayo kwa asilimia nyingi huwa na joto kali hasa majira ya mchana hadi saa 11, likapungua kwa kiasi kikubwa.

Halafu baada ya nusu saa ikaanguka mvua ya 'kufa mtu.' Ni mvua iliwalazimu wauza miamvuli kuzidisha bei mara mbili ya ile ambayo wanauza.

Iliwalazimika wakazi wa Dar kutoka majumbani mwao na miamvuli, wengine masweta na makoti.

Ni kipindi hicho hicho ambacho mmoja wa waliokuwa barabarani wanyeshewa na mvua alikuwa na mwanaume mmoja aliyevaa shati la bluu, suruali nyeusi na viatu vyeusi pia. Alikuwa na mwamvuli mdogo tu ambao haukumzuia kuloana kwani ilikuwa ni mvua iliyoambatana na na upepo. Inasemekana kuwa miamvuli ile ni ya kujikinga na jua.

Na ndiyo maana inaponyesha mvua inayoambatana na upepo, inapinda na mabawa yake kuchomoka. Kuna miamvuli ile mikubwa, mipana ndiyo ambayo watu wanasema ile imetengenezwa kwa ajili ya mvua.

Ilikuwa ni saa 10:00 jioni, lakini hali ya hewa ilisababisha jiji la Dar lionekane ni saa 12:30 au saa 1:00 usiku, kwani hata baadhi ya magari tayari yalikuwa yamewasha taa yalipokuwa yanatembea barabarani.

Mtu yule alikuwa akipiga hatua moja baada ya nyingine kuelekea anakoelekea.

Mtu mwingine alikuwa nyumbani kwake. Alikuwa amepigiwa simu kuwa atafika nyumbani jioni siku hiyo. Na kwa sababu siku hiyo hakuwa na kazi nyingi na mizunguko pia, alirejea nyumbani mapema kumsubiri mgeni wake.

Mara alisikia mlango ukigongwa. Alijua ni mgeni wake, akaenda kufungua.

"Karibu kaka." Akamkaribisha.

"Ahsante, habari za hapa."

"Nzuri tu, karibu sana, unajua umenitisha sana mchana uliponipigia simu kuwa utakuja nyumbani kwangu, maana si kawaida sana. Yaani niko peke yangu halafu uje nyumbani!"

"Ni lazima ikushangaze, ila hakuna chochote kibaya ndugu yangu."

"Hakuna kibaya? Ila kuna kizuri, si ndiyo?" Wote wakaangua vicheko.

Walikuwa ni ndugu wawili, Belo na Dan. Mkubwa ambaye ni Belo alimpigia simu ndugu yake kuwa kama atatoka mapema kazini basi amkute nyumbani kwake.

"Mimi nilijua na mvua hii huwezi kuja, bado kidogo nikupigie simu nikwambie basi kama tuonane kesho nitakuja huko huko nyumbani maana mvua imezidi."

"Dan mvua gani hii ya kusababisha mimi nisije, unajua watu wa Dar tunajiendekeza sana. Kutoka hapo Manzese Tip Top hadi Mabibo?"

Yalikuwa na mazungumzo ya hapa na pale katika ya wanandugu hao, lakini Dan alijua kabisa kuna kitu ambacho huenda kaka yake amekuja kumwambia.

"Mdogo wangu mimi nimekuja hapa maalum kwa ajili ya jambo moja." Belo alizungumza akiwa sasa ametulia. Na hicho ndicho Dan alikuwa akikisubiri.

"Wiki ijayo siku ya Jumapili nina kijipati nyumbani. Yule mwanao Tima, anatimiza miaka mitano sasa tangu kuzaliwa, kwa hiyo nimeandaa kisherehe kidogo cha 'bethdei' yake, kwa hiyo nakuomba usikose nyumbani."

Kwa akili yake Dan hakutegemea hilo. Alidhani huenda kaka yake alikuwa na kitu kikubwa kuliko hicho. Kitendo cha kufunga safari na kwenda nyumbani kumualika rasmi kama mtu baki, kilimshangaza kidogo.

"Sasa kama ni hivyo si ungeniambia tu kwenye simu, yaani umeacha shughuli zako na mvua hii nilidhani jambo ni kubwa sana!"

"Nina maana yangu Dan. Ningekupigia simu na wewe ungechukulia kisimusimu tu, siku hiyo unaweza kupata kijidharura kidogo, ukanipigia simu ukaniambia siji. Lakini hii nimeamua kuja mwenyewe kwa sababu nataka uwepo nyumbani siku hiyo, ni muhimu sana, usikose."

"Sawa kaka mimi nitakuja, wala haina shida."

"Enhe, umepata mwanamke mwingine au?" Lilikuwa ni kama swali la mtego hivi.

Dan akacheka halafu akajibu "Nina hamu na mwanamke kaka? Hili lenyewe limenishinda."

"Sasa si umlete basi yule aliyempigia simu Husna, maana kaharibu halafu hataki kuja kuchukua nafasi."

Maneno hayo yalimfanya kucheka tena. Lakini safari hii ilikuwa ya maumivu ndani yake. Akakumbua alichopitia wiki moja iliyopita.

"We kaka we, yaliyonikuta ni siri yangu mwenyewe. Lakini kwa sababu umenichokoza, ngoja nikwambie. Si nilikwambia nitaenda kwa Ziada. Nilichokipata huko Mungu mwenyewe ndiye anajua.

Aliniruka futi mia kwenda juu, akakataa katakata, halafu akanipakia maneno ya ajabu, we acha tu.

Na kaniambia tayari yeye ana mchumba anataka kuolewa kwa hivyo hawezi kufanya hivyo. Nikatoka hapo, nikaenda kwa mke wangu, bwana wee, yeye na mama yake hawakuniacha bure, walinipakia maneno hayo, nikatoka mbio."

**ITAENDELEA JUMAPILI**

# MISS TANZANIA AJITOSA BINTI KINARA

**Na Halfani Chusi**

Miss Tanzania 2021, Juliana Lugumisa amejitosa kuwa mlezi wa mradi wa binti kinara, unaohusisha kusaidia watoto wa kike wenye uhitaji maalumu ikiwamo elimu.

Amesema ameamua kuunga mkono mradi huo unaoratibiwa na Shilikisho la Vikundi vya Ujasiriamali Tanzania (SHIVUTA), kwa kuwa jambo wanalolifanya linagusa jamiii moja kwa moja.

"Mimi ni mwanataaluma wa viungo bandia, pia ni mwanzilishi wa taasisi ya kusaidia watu wenye ulemavu wa viungo kwa hiyo kuwa kwenye mradi wa kusaidia mabinti kutimiza ndoto zao kwangu ni fahari pia tutakuwa pamoja"aliahidi.





# Nzige Boy kuwachezesha Msaga Sumu, Snura

Msanii wa Bongo Fleva anayefanya vizuri mkoani Tabora, Salehe Hamisi , maarufu kama Nzige Boy anatarajia kutoa singo kali akishirikisha wakongwe wa singeli Msaga Sumu na Snura.

Nzige Boy anayetamba na wimbo wake 'Ndoa', ameliambia BT kuwa anatarajia baada ya kutambulisha ngoma hiyo kukubali jina la Mfalme wa Tabora ambalo wafuasi wake wamempa baada ya kufanya vizuri kwenye tasnia ya muziki.

"Mapema mwezi ujao nitaachia ngoma yangu ambayo nimewashirikisha Msaga Sumu na Snura. Wimbo huu umetengenezwa na Man Jay Killer na utatoka chini ya usimamizi wa Mudy Sundy (M-Sound Lebo) ," amesema Nzige Boy.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### NEYMAR ANUKIA CITY

KLABU ya Manchester United itachukua hatua kumsajili mshambuliaji wa Paris-St Germain na Brazil, Neymar mwenye umri wa miaka 31 iwapo dau kutoka timu ya Qatar, inayoongozwa na Sheikh Jassim, kwa ajili ya klabu litafanikiwa. (***Sun***)

### BELLINGHAM: NAENDA MADRID

KIUNGO wa kati wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19 ameamua kujiunga na Real Madrid, lakini mataba wake bado haujaisha na klabu hiyo ya Hispania ambayo iko tayari kumlipa Euro milioni 120. (***AS***)

### KANE RASMI SOKONI

KLABU ya Tottenham Hotspur inatarajia kupokea dau kutoka kwa Chelsea kwa ajili ya mshambuliaji wa England, Harry Kane, mwenye umri wa miaka 29, huku azma yao ya kumteua Mauricio Pochettino kama kocha ikiendelea kuongezeka. (***Talksport***)

### SPURS: KANE HAUZWI

MWENYEKITI wa Tottenham Hotspur, Daniel Levy, ameshindwa kushawishika hatamuuza, Harry Kane, kwa Manchester United au Chelsea, huku Mashetani Wekundu wakiwa wanamtaka pia mshambuliaji wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen (24), na mshambuliaji wa Juventus na Serbia, Dusan Vlahovic (23), kwenye orodha ya wawachezaji mbadala wa Kane. (***Daily Mail***)

### BALE AIKATAA HOLLYWOON

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Tottenham Hotspur, Real Madrid na Wales, Gareth Bale, mwenye umri wa miaka 33 amekataa ombi kutoka kwa wamiliki wa Hollywoon Wrexham, Ryan Reynolds na Rob McElhenney ya kujiunga na klabu hiyo mpya iliyopanda daraja. (***Sky Sports***)

### MILNER KUTUA BRIGHTON

KLABU ya Brighton inajiandа kuchukua hatua kuhusu mchezaji wa Liverpool, James Milner mwenye umri wa miaka 37, huku mkataba wa kiungo huyo wa kati wa England ukimalizika msimu huu. (***The Athletic***)

### ONANA AKARIBIA CHELSEA

CHELSEA inatafakari kuhusu mkataba wa mabadilishono ya wachezaji kwa ajili ya kumpata mlinda mlango wa Inter Milan, Andre Onana, mwenye umri wa miaka 27. (***Gazzetta***)

### KOVACIC SASA KUUZWA

CHELSEA ingependelea kumuuza kiungo wa kati wa Croatia, Mateo Kovacic, mwenye umri wa miaka 28 kwa klabu iliyo nje ya Ligi Kuu England, huku kocha wa zamani wa Blues hao, Thomas Tuchel akiwa na nia ya kujiunga tena na Bayern Munich. (***Evening Standard***)

### MBAPPE AMTAKA MUANI

MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe, anajaribu kumshawishi mshambuliaji wa Eintracht Frankfurt na mchezaji mwenzake wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Randal Kolo Muani, mwenye umri wa miaka 24 ajiunge na PSG msimu huu. (***Christian Falk***)

### KANTE ATAJWA ARSENAL

ARSENAL inaangalia uwezekano wa kuchukua hatua ya kuhamisho kwa ajili ya kiungo wa kati wa Chelsea na Ufaransa, N'Golo Kante, mwenye umri wa miaka 32, huku washikabunduki hao wakijua mahasimu wao wa London wanahitaji kupunguza ukubwa wa kikosi chao. (***Mirror***)

### DAVID KUONDOKA LILLE

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Canada, Jonathan David, mwenye umri wa miaka 23, anatarajiwa kuondoka katika klabu ya Ufaransa ya Lille msimu huu, ambayo imezifahamisha timu mbalimbali zikiwamo Tottenham Hotspur, Chelsea na Paris St-Germain. (***L'Equipe***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA AIPOTEZEA REAL MADRID ULAYA

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola anajaribu kila awezalo kuipuuza Real Madrid wakati timu yake ya Manchester City ikijaribu kupambana katika vita ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England.

**City itamenyana na Fulham, West Ham na Leeds United kabla ya kusafiri hadi Madrid kwa ajili ya mchezo wao wa kwanza wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya utakaochezwa Mei 9, mwaka huu.**

Ubingwa uko mikononi mwao kufuatia ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Arsenal walioupata Jumatano iliyopita, lakini Guardiola amesisitiza hajatulia kiasi cha kuanza kupata wasiwasi kuhusu Madrid.

"Nina wazo la mpango dhidi ya Real Madrid kwa ukweli tulicheza msimu uliopita," alisema Guardiola katika mkutano wa waandishi wa habari.

"Wakati mwingine katika mwaka ninaona Ligi Kuu Hispania. Walibadilisha baadhi ya mambo kutoka msimu uliopita, lakini ni kocha yule yule. Kawaida mimi huwa na wasiwasi kuhusu mchezo unaofuata. Sizingatii chochote isipokuwa Fulham."

**Afunguka kwa sasa anaangalia mechi muhimu za EPL ambazo zinaweza...**

City wamebakiza mechi tatu pekee ili washinde Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza katika historia yao na wanaweza pia kulipiza kisasi cha kufungwa na Madrid katika hatua ya nusu fainali msimu uliopita.

Kinyume chake, wameshinda Ligi Kuu katika miaka minne kati ya mitano iliyopita na mara sita tangu 2012.

"Unapokuwa na pointi 10 au 15 nyuma ya kiongozi, unaweza kutanguliza Ligi ya Mabingwa Ulaya," Guardiola aliongeza.

"Hatuna muda wa kutanguliza chochote, Ligi Kuu inavutia sana, nzuri sana. Watu wanasema kwa nini, sio kweli lakini Ligi Kuu ni Ligi Kuu, ni miezi 11 kila wiki. Mawazo yangu ni Fulham halafu West Ham, baadaye Leeds. Baada ya Leeds, si muda mwingi lakini tuna muda wa kujiandaa kwa Madrid."

Baada ya ushindi dhidi ya Arsenal, City iko nyuma ya vinara hao kwa tofauti ya pointi mbili, lakini wakiwa na michezo miwili mkononi.

Wamechukua faida ya timu ya Mikel Arteta kuchukua pointi tatu pekee kutoka katika a michezo minne iliyopita, lakini Guardiola amesisitiza jambo hilo linaweza kutokea kwa City.

"Namfahamu vyema Mikel na wachezaji wanafahamu hilo, hawatakata tamaa," alisema Guardiola.

"Hawatakata tamaa. Ukweli leo tupo nyuma kwa pointi mbili. Tuwe na heshima kwa timu tunazocheza, lazima tuzifunge. Ukweli ni tuko nyuma.

"Siku zote nasema mbele ya Arsenal, kilichowapata kinaweza kutokea kwetu. Haiwezekani? Hapana, inawezekana. Unaweza kuangusha pointi ndani ya wiki moja. Tunapaswa kufahamu hilo."

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI

MANCHESTER UTD
VERSUS
ASTON VILLA

1 | 1.82
X | 3.68
2 | 4.11

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MARTINEZ AIPELEKA VILLA ULAYA




**LONDON,** England

EMI Martinez anataka kuona Aston Villa ikifuzu kucheza mashindano ya Ulaya ambayo kwake ni mafanikio makubwa katika soka, kwa mujibu wa kocha wa zamani wa makipa wa Villa, Neil Cutler.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia na Copa America akiwa na Argentina, Martinez anatafuta kuisaidia Villa kurejea Ulaya kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2010.

Wamefurahia mabadiliko ya haraka tangu Kocha, Unai Emery, alipochukua usukani Novemba, mwaka jana, huku wakicheza mechi 10 bila kupoteza kwenye Ligi Kuu kukiwapandisha hadi nafasi ya sita mbele ya Manchester United.

Cutler mwenye umri wa miaka 46, alisifia kiwango cha Martinez na kusema anafurahia kufuzu kucheza Ulaya.

Na kocha huyo mwenye sifa ya juu ameisitiza mtetezi wake wa zamani analenga kutengeneza soka la bara na vipengele vya fedha mara kwa mara pale Villa Park.

Aliiambia LiveScore: "Martinez ni mmoja wa makipa bora, ikiwa sio bora zaidi, ulimwenguni. Anataka kushinda mashindano, anataka kupata mataji, anataka kutwaa medali."

# Sheikh Al-Thani na ofa ya United



**MANCHESTER,** England

SHEIKH Jassim bin Hamad Al-Thani aliwasilisha ombi lake la tatu na la mwisho la kuinunua Manchester United juzi na anabakia na imani litafanikiwa licha ya wasiwasi ambao wamiliki wa sasa, familia ya Glazer, wamedhamiria kusalia, vyanzo vimeiambia ESPN.

Raine Group, benki ya mfanyabiashara inayoshughulikia mchakato wa Glazers, ilikuwa ikitarajia awamu ya tatu ya ofa siku ya Ijumaa.

Zabuni kutoka kwa Sheikh Jassim imeungwa mkono na Qatar ingeondoa deni lote na inajumuisha namba ya kununua klabu pamoja na uwekezaji wa ziada wa mtaji na miundombinu, vyanzo viliongeza.

INEOS, inayoongozwa na bilionea wa Englabd, Sir Jim Ratcliffe, pia iliwasilisha zabuni mpya kabla ya tarehe ya mwisho, wakati mapendekezo yatatolewa na makundi yanayotaka kununua hisa za wachache ikiwa ni pamoja na Elliott Management, Ares Management Corporation, Sixth Street na Carlyle.

Vyanzo vimeiambia ESPN kuwa INEOS wamejadili ofa ambayo ingewajumuisha Joel na Avram Glazer, ndugu wawili waliohusika sana Old Trafford, kuhifadhi hisa katika klabu - hatua ambayo tayari imesababisha upinzani mkubwa kutoka kwa mashabiki.

Sheikh Jassim ameonyesha nia ya kununua asilimia 100 ya hisa na kukamilisha umiliki kamili na kuna imani ndani ya muungano wake ofa hiyo itakuwa na faida kubwa ya kuwashawishi Glazers kuuza.

## HABARI MICHEZO

CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

# Mwembeladu yajitabiria neema ikiivaa Kundemba

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Mwembeladu FC imesema imejipanga vyema kuhakikisha inatimiza malengo yake kwa kusonga mbele katika mashindano ya Kombe la FA yanayoendelea visiwani hapa, imefahamika.

Kikosi hicho kinatarajia kuvaana na Kundemba katika mechi ya kwanza ya hatua ya robo fainali ya Kombe la FA itakayochezwa leo kuanzia saa 10:00 jioni kwenye Uwanja wa Amaan.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Juma Mohammed, aliliambia gazeti hili wanafahamu mchezo huo utakuwa mgumu na wenye ushindani kutokana na kila upande kujiandaa vyema.

Mohammed alisema wachezaji wake wana hamasa kubwa kuelekea mchezo huo na amejiandaa kukutana na changamoto kutokana na aina ya wapinzani wanaokutana nao.

"Tuko tayari kwa mechi, tunajua haitakuwa rahisi, timu zote mbili zinajuana na hali hii ya ushindani huongezeka pindi zinapokutana klabu zinazocheza daraja tofauti," alisema Mohammed.

Kocha huyo alisema licha ya wapinzani wao kushiriki Ligi Kuu Zanzibar na wao Mwembeladu wanachuana katika Ligi ya Mkoa, haimaanishi watashindwa kupambana hadi kupata ushindi. "Tunashuka uwanjani kwa ajili ya kupambana kupata ushindi, tunajua mechi itakuwa ngumu na yenye kujaa hamasa ya ushabiki kwa timu zote lakini hamasa ya mashabiki ndio itakayopelekea ushindi kwetu," alisema kocha huyo.

Naye Meneja wa Kundemba, Ramadhani Suleiman, alisema kikosi chao kimeandaliwa vyema kukabiliana na ushindani na ukubwa na mechi hiyo.

Suleiman alisema walianza maandalizi mapema na wanawasisitiza wachezaji wao kujituma wakati wote ili kuvuna matokeo chanya.

Bingwa wa michuano hiyo atazawadiwa kitita cha Sh. milioni 30 kutoka wadhamini wa Kuu wa Ligi Kuu Zanzibar ambao ni Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ).



Mchezaji wa gofu, Arshid Esmail, akipiga mpira katika mashindano ya Kumbukumbu ya Galinoma yaliyofanyika kwenye viwanja vya Lugalo, Dar es Salaam jana. Kampuni ya magazeti ya The Guardian Limited ni moja ya wadhamini wa mashindano hayo ya mwaka huu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Yanga SC yawaita wananchi*

INATOKA UK 24

anawafatilia kwa karibu mechi zote za kimataifa.

Kocha wa Rivers United, Stanley Azunda Eguma, alisema walipoteza nyumbani kwao na inamaanisha zilikuwa dakika 90 za faida kwa Yanga huko Nigeria na sasa wako Tanzania kumalizia dakika 90 nyingine zilizobakia.

Eguma alisema amefanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika mechi ya awali na sasa amejiandaa kupambana ili kupata matokeo mazuri ugenini na katika soka hilo linawezekana.

"Tumejiandaa vizuri na sasa tumekuja kwa ajili ya kutafuta ushindi katika mchezo huu kwa kufunga idadi kubwa ya mabao licha ya kukabiliwa na majeruhi, katika mchezo wa kesho (leo) hauwezi kuwa mwisho hadi iwe mwisho," alisema Eguma.

Nyota wa Rivers United, Festus Austin, alisema wamepoteza nyumbani na sasa wako hapa kusahihisha makosa yao.

"Tumejiandaa kwa njia yoyote ile haijalishi timu za Tanzania kutumia vyema uwanja wao wa nyumbani, tumejipanga kwa dakika 90 kutafuta matokeo mazuri," alisema mchezaji huyo.

## Simba : Tunastahili gwaride la heshima

INATOKA UK 24

timu pekee zenye uwezo wa kutucheka sisi ni wale watakofuzu nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika waliobaki wote Afrika, hii wanatakiwa watupigie gwaride la heshima," alisema Ahmed.

Mwaka 2019 Simba ilitolewa katika hatua hiyo kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), ikifungwa ugenini mabao 4-1, baada ya suluhu ya nyumbani na mwaka juzi ilichapwa magoli 4-0 na Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini, licha ya ushindi wa mabao 3-0 walioupata nyumbani.


## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAPILI - 30/04/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 3530 | Inter vs Lazio | 1.81 | 3.58 | 4.28 |
| 14:00 | 5274 | Monaco vs Montpellier | 1.49 | 4.57 | 5.56 |
| 14:00 | 5307 | Cardiff vs Huddersfield | 2.29 | 3.18 | 3.18 |
| 14:30 | 2417 | Holstein Kiel vs SV Darmstadt | 3.03 | 3.67 | 2.16 |
| 14:30 | 3062 | Fortuna Dusseldorf vs Karlsruher SC | 1.93 | 3.78 | 3.53 |
| 15:00 | 3463 | Cadiz CF vs Valencia | 2.99 | 3.14 | 2.43 |
| 15:15 | 2072 | FC Zurich vs FC Sion | 1.65 | 3.89 | 4.94 |
| 15:30 | 2726 | Mechelen vs Royal Antwerp | 4.17 | 3.59 | 1.85 |
| 15:30 | 5217 | Rangers FC vs Celtic | 3.03 | 3.39 | 2.22 |
| 16:00 | 1068 | Manchester Utd vs Aston Villa | 1.82 | 3.68 | 4.11 |
| 16:00 | 2057 | Newcastle vs Southampton | 1.32 | 5.18 | 8.97 |
| 16:00 | 2098 | Cremonese vs Verona | 3.03 | 3.23 | 2.35 |
| 16:00 | 2474 | Fulham vs Manchester City | 9.90 | 5.40 | 1.28 |
| 16:00 | 2693 | Rennes vs Angers | 1.29 | 5.34 | 9.09 |
| 16:00 | 3783 | Sassuolo vs Empoli | 1.74 | 3.90 | 4.29 |
| 16:00 | 3956 | Bournemouth vs Leeds | 2.58 | 3.37 | 2.63 |
| 16:00 | 4025 | Troyes vs Nice | 4.35 | 3.81 | 1.73 |
| 16:00 | 4894 | Clermont Foot vs Reims | 2.92 | 3.47 | 2.28 |
| 16:30 | 1216 | Bayern Munchen vs Hertha BSC | 1.11 | 9.16 | 17.92 |
| 17:15 | 3702 | Real Oviedo vs Ponferradina | 2.13 | 3.03 | 3.78 |
| 17:15 | 4622 | Villarreal vs Celta Vigo | 1.81 | 3.65 | 4.20 |
| 17:15 | 5069 | Spal vs Perugia | 2.31 | 3.14 | 3.19 |
| 17:15 | 5249 | Cagliari vs Ternana | 1.78 | 3.58 | 4.47 |
| 17:30 | 1087 | FC Winterthur vs FC Basel | 3.42 | 3.58 | 2.03 |
| 17:30 | 2209 | GD Estoril vs Santa Clara | 2.23 | 3.21 | 3.27 |
| 17:30 | 5141 | BSC Young Boys vs FC Luzern | 1.56 | 4.43 | 5.06 |
| 18:00 | 2820 | Sandefjord vs Aalesunds | 2.34 | 3.30 | 2.99 |
| 18:00 | 3002 | Stromsgodset vs Tromso | 2.31 | 3.42 | 2.95 |
| 18:00 | 4210 | Molde vs Stabaek | 1.41 | 4.84 | 6.73 |
| 18:00 | 4721 | Viking vs Ham-Kam | 1.62 | 3.94 | 5.15 |
| 18:00 | 4885 | Haugesund vs Sarpsborg | 2.59 | 3.37 | 2.61 |
| 18:05 | 5941 | Paris St Germain vs Lorient | 1.20 | 6.79 | 11.33 |
| 18:30 | 2343 | Liverpool vs Tottenham | 1.50 | 4.68 | 5.38 |
| 18:30 | 2562 | Degerfors vs Djurgardens IF | 4.10 | 3.73 | 1.81 |
| 18:30 | 2681 | VfL Wolfsburg vs Mainz | 2.25 | 3.46 | 2.97 |
| 19:00 | 3404 | Besiktas vs Galatasaray | 2.63 | 3.49 | 2.51 |
| 19:00 | 3555 | Ajax vs PSV Eindhoven | 2.29 | 3.48 | 2.86 |
| 19:00 | 3663 | Hajduk Split vs Dinamo Zagreb | 3.36 | 3.41 | 2.09 |
| 19:00 | 4842 | Fiorentina vs Sampdoria | 1.29 | 5.38 | 9.36 |
| 19:00 | 5771 | Lokomotiv Moscow vs FK Khimki | 1.42 | 4.83 | 6.52 |
| 19:30 | 1250 | Granada vs Eibar | 2.12 | 3.18 | 3.58 |
| 19:30 | 3751 | Espanyol vs Getafe | 2.41 | 2.98 | 3.18 |
| 19:30 | 5464 | Racing Genk vs Brugge | 2.30 | 3.59 | 2.85 |
| 20:00 | 2479 | FC Porto vs Boavista | 1.20 | 6.31 | 13.68 |
| 20:15 | 4670 | Odd Ballklubb vs Rosenborg | 2.68 | 3.36 | 2.53 |
| 21:45 | 4965 | Bologna vs Juventus | 3.24 | 3.09 | 2.31 |
| 21:45 | 5515 | Marseille vs AJ Auxerre | 1.29 | 5.37 | 9.14 |
| 22:00 | 1841 | Zaragoza vs Las Palmas UD | 2.54 | 3.03 | 2.93 |
| 22:00 | 5039 | Valladolid vs Atletico Madrid | 4.88 | 3.93 | 1.65 |
| 22:30 | 4988 | Sporting Lisbon vs Famalicao | 1.31 | 5.27 | 9.07 |

Michezo
Nipashe
Jumapili Aprili 30, 2023



Guardiola aipotezea Madrid Ulaya

UK. 21

# YANGA SC YAWAITA WANANCHI

## ●●● Yatamba wako kamili kuandika historia CAF ingawa Nabi akiri wataingia...

**Na Saada Akida**

WAWAKILISHI pekee wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa, Yanga leo wanatarajia kuandika historia ya kutinga hatua ya nusu fainali ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika endapo wataiondoa Rivers United kutoka Nigeria.

**Yanga watawakaribisha Rivers United kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 2-0 waliopata ugenini, hivyo wanatakiwa kukamilizia kibarua walichokianza.**

Kuelekea mchezo huo, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, alisema anafurahi hatua waliyofikia na wamejipanga kutinga dimbani kwa umakini kwa ajili ya kusaka ushindi na kusonga mbele katika mashindano hayo.

Nabi alisema watacheza kwa kujituma na ushindi wa ugenini hautawafanya wasijitume kwa sababu hawataki kujipa presha.

Kocha huyo alisema historia ya baadhi ya timu kushinda ugenini na baadaye kuondolewa wakiwa nyumbani ni somo kubwa kwao linalowafanya watambue wanatakiwa kupambana wakati wote wa mechi.

"Mimi, benchi langu la ufundi pamoja na wachezaji tumekaa na kuwaeleza bado hatujafuzu kucheza nusu fainali kwa sababu kesho (leo) kupata ushindi tena baada ya dakika 90 dhidi ya Rivers United ndio tutaweka historia ya kufuzu kusonga mbele na kufuzu hatua nusu fainali. Hakuna mchezaji atakayekosa katika mchezo wetu dhidi ya Rivers United kwa sababu ya majeruhi, nitakachokifanya, nitafanya kama wanavyofanya makocha wengi, kufanya mabadiliko ya kikosi kulingana na ninavyowaona wachezaji wangu katika mazoezi," alisema Nabi.

Aliongeza mabadiliko atakayofanya yataendana na mfumo atakaoingia nao lakini pia ukitokana na ripoti ya mazoezi kwa kila mchezaji kwa sababu baadhi wanahitaji kupumzika kutokana na kucheza mfululizo.

"Tuko makini, tutaingia katika mechi hii kwa tahadhari kubwa, tutacheza kwa aina mbili, tutazuia endapo wapinzani wakiwa na mpira na tutashambulia sisi tunapokuwa na mpira, lakini siwezi kuweka wazi ni mfumo gani nitaingia nao kesho (leo),lakini tumejipanga vizuri, hatutawaangusha," Nabi alisema.

Kiungo wa Yanga, Zawadi Mauya, alisema wachezaji wako vizuri na wamejiandaa kukabiliana na Rivers United kwa tahadhari kwa sababu hawataki kutolewa katika mashindano hayo na wanasubiri kuandika historia ya kucheza hatua ya nusu fainali.

"Kitu kikubwa ni kutaka kuvuka hatua hii, awali hatukuwa vizuri katika michuano hii kwa miaka ya nyuma, ila kwa kuvuka hatua hii itakuwa ni historia, tunahitaji kuendelea kwa kuvuka hatua ya robo na kucheza nusu fainali ya Afrika," alisema Mauya.

Aliongeza licha ya ahadi za motisha zinazotolewa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, lakini wanahamasika zaidi kuona kiongozi huyo mkuu wa nchi

INAENDELEA UK 23



Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi.

## Simba : Tunastahili gwaride la heshima

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kutolewa katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba imetamba kuweka heshima kwa sababu walikuwa ni wawakilishi pekee wa Afrika Mashariki na Kati waliofika hatua ya robo fainali katika michuano hiyo.

Simba iliondolewa na Wydad AC ya Morocco baada ya kufungwa penalti 4-3 kutokana na matokeo ya jumla kumalizika kwa sare ya bao 1-1.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema ingawa timu yao 'imefeli' na kushindwa kutimiza malengo, lakini wanafurahu kuweka heshima kubwa kama klabu, nchi na Afrika Mashariki na Kati kwa ujumla.

"Tumefeli, hatujatimiza malengo, lakini tunajivunia timu yetu, tunajivunia maendeleo ya timu yetu. Heshima tuliyoiweka Afrika haina mfano wake, kumbukumbu mbaya tuliyoiacha Morocco hawataisahau daima, Mwana- Simba tembea kifua mbele, kiwango cha timu yetu ni cha juu sana, hakuna timu yeyote katika ukanda wetu imefikia hata theluthi," alisema Ahmed.

Aliongeza kwa sasa Simba inacheza mpira wa kiwango cha juu na kitu pekee ilichozidiwa na timu kubwa ni mataji ambayo wameshayapata.

"Kuna nyakati ilikuwa ukiangalia mechi za Waarabu unasema wenzetu wako mbali sana, niwaambie tu huko mbali na sisi Simba tumeshafika, tunazidiwa na timu kubwa za Afrika mataji, lakini ubora wa timu zetu hatupishani," Ahmed alisema.

Aliongeza klabu pekee ambazo zinatakiwa kuwabeza ni zile ambazo zitafuzu hatua ya nusu fainali tu na zilizobaki hazina haki hiyo na kuwahakikishia wanachama na mashabiki wa Simba mafanikio ya klabu yao kwa sasa hayako mbali.

"Tumecheza robo fainali kwa kiwango cha fainali, hii maana yake timu yetu ina hadhi ya nusu fainali au fainali, mafanikio yetu hayako mbali,

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >